




**Simulizi** machungu aliyepata ajali gari miaka 20 iliyopita

UKURASA 4

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa



ZUCHU KWA KUZUGA BALAA

UKURASA 20

Jumapili Agosti 21, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0581044
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Kilio uhaba wa mahindi

• **Wafanyabiashara** wadaiwa kuyanunua na kuyaficha, bei yapanda ghafla... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### KIGOGO ALIYELALAMIKIWA SASA ASIMAMISHWA KAZI

SERIKALI imemsimamisha kazi Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani Tabora, Absalom Cheliga, kupisha uchunguzi wa tuhuma...

UKURASA WA 3

### ALIYEDAIWA KUMUUA MAMA AACHIWA HURU



WENDY Mrema, aliyekuwa akikabiliwa na kesi ya mauaji ya mama yake mzazi, ofisa muuguzi wa zamani wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini (KCMC), Patricia...

UKURASA WA 4

### MWANAFUNZI AJINYONGA KISA KUUNGUA KWA SARE ZA SHULE

MWANAFUNZI wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Maleutsi wilayani Makete, Marko Sanga (12) amekutwa amejinyonga kwa kutumia...

## Nape asema hakuna wizi vifurushi vya simu

UKURASA 3



Naibu Spika wa Bunge, Mussa Zungu (kushoto), akiongoza matembezi ya hiari yaliyoandaliwa na Diwani wa Kivukoni, Sharik Choughule (wa pili kushoto), jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kuhamasisha wananchi kushiriki Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika nchi nzima Jumanne ijayo. **PICHA: JUMANNE JUMA**



## Shaka anusa harufu ufisadi bilioni 1.6/-

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA YATAKATA KWA COASTAL** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Mkazi wa Dar es Salaam, akiwa amepumzika kwenye kituo cha daladala cha njiapanda ya Bahari Beach jana, huku paa la kituo hicho, likihatarisha usalama wa abiria. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kilio uhaba wa mahindi

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI serikali ikiweka mikakati ya kukabiliana na baa la njaa, kimeibuka kilio cha uhaba wa nafaka hususan mahindi katika mikoa mbalimbali nchini.

Hali hiyo inadaiwa kutokana na baadhi ya wafanyabiashara kuyanunua na kuyahifadhi wakisubiri bei ipande ili wapate faida.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe umebaini pia baadhi ya wafanyabiashara kutoka nchi za jirani nao wanaonekana vijijini wakiyanunua kwa wingi na kuyasafirisha.

Mwanzoni mwa mwezi huu, Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa katika ziara ya kikazi Mbeya, Njombe na Iringa, aliwataka Watanzania kuweka akiba ya chakula ili kuepuka kukumbwa na baa la njaa. Rais alisema Tanzania imeanza mikakati ya kukabiliana na baa la njaa lililotokana na na athari za UVIKO-19 duniani.

Mfanyabiashara kutoka Katesh mkoani Manyara, Clement Fissoo, aliiambia Nipashe jana kuwa kuna baadhi ya wafanyabiashara wanaonunua mahindi na kuyahifadhi wakisubiri bei ipande ndipo wayauze.

Alisema kwa sasa bei ya mahindi wilayani humo ni Sh. 90,000 kwa gunia na yanapatikana kidogo huku akibainisha kuwa kumekuwa na wafanyabiashara kutoka nchi jirani ya Kenya wanaoingia vijijini kununua mahindi.

Katibu wa Soko Kuu la Babati, Rashid Ngula, alisema wafanyabiashara wa kutoka nchi jirani wameathiri soko la mahindi kwa sababu awali walikuwa wakinunua gunia la kilo 100 kwa Sh. 50,000 lakini sasa linauzwa Sh. 90,000.

Ngula alisema mfanyabiashara mmoja wa nchi hiyo ya jirani akienda vijijini, ananunua magunia 200, hivyo kuiomba serikali kuingilia kati ili kutokuibuka baa la njaa.

Mfanyabiashara wa mahindi Mbalizi mkoani Mbeya, Queem Mlowe, alisema baada ya Rais Samia kutoa tahadhari kuhusu uhaba wa chakula, mahindi yameadimika kutokana na wakulima wengi kuacha kuuza.

Alisema wakulima wamekuwa wakiyakusanya kutoka kwa wakulima na kuwauzia matajiri ambao wanapeleka Dar es Salaam na Nairobi, Kenya.

Naye Barick Mwaikambo alisema kutokana na kuadimika kwa mahindi, kuna hatari ya bei kupanda zaidi katika kipindi hiki, hivyo kusababisha biashara kuwa ngumu zaidi.

Alisema mwaka jana kipindi kama hiki, walikuwa wananunua mahindi kati ya Sh. 5,000 na 6,500 kwa debe lakini sasa bei imefika Sh. 14,000. Tangu Rais Samia atoe tahadhari, alisema wakulima wengi wameacha kuuza na wale wanaoyauza wanafanya kwa kiwango kidogo.

"Kipindi kama hiki wakulima huuza mahindi kupata fedha za maandalizi ya mashamba, lakini kwa sasa wengi hawauzi," alisema.

Meneja wa Soko la Kimataifa la Mazao la Kibaigwa mkoani Dodoma, Emanuel Kereyani, alisema hivi karibuni wafanyabiashara kutoka Kenya walikuwa wakiingia kwa kasi vijijini na kununua mahindi.

"Lakini kwenye soko letu hatuna uhaba mkubwa kwa sababu mazao yanaingia kila siku, kwa sasa tupo kwenye msimu wa mahindi yanaingia kwa wingi lakini bei imekuwa kubwa."

Mfanyabiashara katika soko la Mpanda Hoteli, Stumai Jafari, aliliambia gazeti hili kuwa kwa sasa biashara ya mahindi hairidhishi kwa soko la ndani la mkoa wa Katavi ikilinganishwa na kipindi cha nyuma.

Alisema hilo ndilo linalowafanya wafanyabiashara kutafuta soko nje ya mkoa wao baada ya bei mkoani humo kuonekana kuzorota, hivyo kuona afadhali kuuza nje ya mkoa.

Mfanyabiashara mwingine sokoni hapo, Peter James alisema mahindi mengi kwa sasa wanayatoa Sumbawanga mkoani Rukwa kutokana na uchache wa bidhaa hiyo uliopo Katavi.

"Jioni ukikaa barabarani utaona magari yakiwa yamebeba mahindi, hata kule Stesheni yamekwenda kuna mabehewa yamebeba. Magari yakitoka hapa yanapita vijijini yanapakia kwa mfano Majimoto," James alisema.

**RUVUMA WAPAZA SAUTI**

Baadhi ya wakulima wilayani Songea mkoani Ruvuma, wameiomba serikali kuwadhibiti wafanyabiashara wanaopita vijijini kununua mahindi kwa bei ya chini ambayo hailingani na gharama za uzalishaji.

Mkazi wa Kijiji cha Mgazini, Elisha Komba, alisema bei ya mahindi ya serikali kwa hivi sasa katika kata ya Mgazini ni kati ya Sh. 650 mpaka Sh. 700 kwa kilo na wafanyabiashara wananunua Sh. 640 kwa kilo.

**ASKOFU AONYA**

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, amewasihi Watanzania kuacha 'kiburi' cha kuuza ovyo mazao ya nafaka, hasa mahindi kwa ajili ya kutengeneza vilevi.

Askofu Shoo amewataka waweke akiba ili kujinusuru na baa la njaa, litakalosababisha kuwapo kwa mfumuko wa bei ya vyakula nchini.

Kiongozi huyo alitoa tahadhari hiyo kupitia taarifa iliyochapishwa na kuwekwa katika akaunti ya mitandao ya kijamii ya Dayosisi ya Kaskazini, baada ya kumalizika Mkutano Mkuu wa 37 wa tathmini ya utendaji na miradi.

"Nitoe rai kwa jamii, kuweka akiba ya chakula kidogo kilichopatika kutokana na ukame uliosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. Hii ni tahadhari kwa wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro, na nchi nzima kwa ujumla wake," ilisema taarifa hiyo.

Ofisa wa Wizara ya Kilimo, ambaye hakutaka jina lake litajwe, alipoulizwa kuhusu jambo hilo, alisema kama kuna mfanyabiashara anafanya ndivyo sivyo, anatakiwa kuripotiwa kwenye mamlaka za serikali ngazi ya wilaya au mkoa.

"Hakuna mtu aliyekatazwa kwenda kununua mahindi. Tunachokataa ni ama asinunue mahindi kwenye vipimo ambavyo si sahihi au kuweka rumbesa akamnyonya mkulima. Kama kuna mtu mwenye taarifa mtu kanunua mahindi halafu ameyaficha hicho ni kitu kingine.

"Kwa huku ngazi ya wizara ukiuliza jambo la Mufindi inakuwa kidogo kuna changamoto maana kule kuna Mkuu wa Wilaya, kuna Mkurugenzi unamwambia kuna mtu fulani anaficha," alisema.

■**Imeandaliwa na Agusta Njoji (Dodoma), Neema Hussein (Katavi), Godfrey Mushi (Arusha), Mary Mosha (Moshi), Jaliwason Jasson (Manyara), Zanura Mollel (Namanga), Nelbart Msokwa (Mbeya) na Gideon Mwakanosya (Ruvuma).**

# Shaka anusa harufu ufisadi wa bil. 1.6/-

**Na Beatrice Shayo,** TABORA

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, ameshtukia ufisadi wa Sh. bilioni 1.6 za ujenzi wa bwawa la umwagiliaji mkoani Tabora.

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, Shaka ameagiza kuchukuliwa hatua dhidi ya watu wote waliohusika na ubadhirifu huo.

Shaka alishtukia jambo hilo na kutoa maagizo juzi katika ziara yake mkoani hapo alipotembelea bwawa hilo mahususi kwa shughuli za kilimo katika kijiji cha Inara, Manispaa ya Tabora na kusikiliza kero za wananchi.

Wananchi walimweleza kiongozi huyo kuwa kuna viongozi wamewafanyia usanii kwa kuwa mradi huo hauna uhalisia wa fedha zinazotajwa kutumika kwa kuwa wanaweza kutembea kwa miguu bila kuzama.

Shaka alisema changamoto kubwa ambayo inaonekana katika fedha hizo, matokeo halisi hayaonekani, hivyo watu waliohusika watafutwe na kuchukuliwa hatua.

"Mkurugenzi (wa manispaa) watafute hao waliopiga hizi Sh. bilioni 1.6 ni hela ndefu ya serikali wamekula na wamejenga mradi hauna kiwango hata mafanikio yake hayaonekani kwa wananchi. Huu ni ujanja ujanja umefanyika.

"Huu ni ubadhirifu mkubwa nadhani tuwatafute waliohusika. Hatuwezi kufumbia macho jambo hili na pia kuna jambo lipo watumishi wa halmashauri wamejichukulia maeneo hapa," alisema huku akibainisha kuwa kuna baadhi ya watumishi wanaogombania maeneo huku watumishi wakiwa wamejichukulia maeneo na kuwapangisha.

"Mkurugenzi anzeni na watumishi wenu waliojichukulia maeneo kwa wananchi na myarudishe kwa wananchi. Mimi nina orodha mkitaka niwasaidie nitawapatia na miongoni mwao wamekuja kuwakodishia watu. Hii si sahihi, Sh. bilioni 1.6 wamepiga, maeneo wamechukua hii sasa kiboko," alisema Shaka huku akisema watu hao wanadumaza jitihada za maendeleo na wamechangia kwa namna moja kwa mradi kukwama.

Shaka aliweka bayana kwamba chama hakiwezi kulifumbia macho suala la Sh. bilioni 1.6 na kwamba kitalifuatilia hadi dakika ya mwisho ili kujua hatua gani zilizochukuliwa.

"Mkurugenzi tutasubiri utupatie taarifa ni watu gani waliohusika na ubadhirifu huu wa fedha nyingi za serikali kujenga mradi ambao uko chini ya kiwango na kujenga mradi ambao hauna tija kwa wananchi," alisema Shaka.

"Wakati huo huo kuna fedha zilizotengwa kwa mwaka 2022/23 nazo zinakuja hapa. Sijui kwa kweli usalama wa hiyo fedha utakuwaje. Kama hela ya kwanza mradi umeenda juu kwa juu na mradi hauna kiwango na hata mbunge wenu ameeleza," alisema.

"Jambo hilo linasikitisha kama hiyo ni aina ya miradi ya maendeleo inayosimamiwa. Imenibidi niwe mpole kama nimechomwa sindano na hawa wananchi wanazungumza kwa hisia na mwaka huu katika bajeti, Rais Samia ametenga Sh. bilioni 400 kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji," alisema.

Shaka pia alionya kwamba fedha zinazotolewa na Rais Samia si za mjomba wala sadaka ndiyo maana wanazifuatilia kwa umakini ili kujua uhalisia wa fedha na matumizi yake katika miradi iliyopangwa.

"Hakuna fedha ambayo itapotea. Tulikuja tukaomba dhamana kwa wananchi na tuliahidi kuwa tutawaletea maendeleo. Kasi ya kuleta maendeleo inafanywa vizuri lakini wako watumishi ambao si waadilifu, wanadumaza jitihada hizi. Hatuwezi kumvumilia yeyote mwenye nia au dhamira ya kukatiza jitihada za kuwaletea wananchi maendeleo," alisisitiza.

"Nikienda Dodoma nipatiwe ripoti iliyonyooka ya huu mradi jitihada na hatua ambazo zimechukuliwa. Serikali ya Rais Samia (Suluhu Hassan) inasimama na ninyi wananchi," alisema Shaka.

Awali Mbunge wa Tabora Mjini (CCM), Emmanuel Mwakasaka, alisema fedha iliyotengwa katika mradi huo haiendani na uhalisia wa bwawa na wananchi hawanufaiki nao. Alisema yako maboresho mengi yalitakiwa kufanyiwa kazi matokeo yake waliohusika hawakufanya licha ya kupewa fedha hizo.

# Aliyedaiwa kumuua mama aachiwa huru

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WENDY Mrema, aliyekuwa akikabiliwa na kesi ya mauaji ya mama yake mzazi, ofisa muuguzi wa zamani wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini (KCMC), Patricia Ibrek (66), ameachiwa huru, baada ya kusota gerezani kwa zaidi ya siku 240.

Juzi, Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, ilimwachia huru Wendy, baada ya upande wa mashtaka katika kesi hiyo, kuwasilisha ombi la kutokuwa na nia ya kuendelea na shauri hilo.

Akisoma uamuzi huo, Hakimu Mkazi Mwandamizi Naomi Mwerinde, alisema mahakama hiyo imekubaliana na ombi la upande wa mashtaka, hivyo imeamua kuwaachia huru mshtakiwa wa pili (Wendy) na mshtakiwa wa tatu, Waziri Ally.

Mshtakiwa wa kwanza katika kesi hiyo ya mauaji ya kukusudia, Omary Mohamed, ambaye ni mganga wa kienyeji, ataendelea na shtaka hilo.

Ombi la kuwafutia mashtaka washtakiwa hao, liliwasilishwa mahakamani humo na Wakili wa Serikali, Nitike Emanuel.

Wakati anawasilisha ombi hilo, Wakili Nitike, alidai kuwa kutokana na mwenendo wa shauri hilo, upande wa mashtaka hauna nia ya kuendelea na shauri hilo kwa mshtakiwa wa pili na wa tatu.

Awali, katika hati ya mashtaka, ilidaiwa mahakamani humo kuwa, Wendy, akiwa yeye na washtakiwa wenzake wawili ambao ni waganga wa kienyeji, Omari na Waziri, walimuua kwa makusudi, Patricia na kisha kumzika kwa siri shambani mama yake mzazi.

Mwili wa marehemu, ulizikwa shambani karibu na nyumba yake mwaka jana na uligunduliwa na majirani zake mwezi Januari mwaka huu.

Ilidaiwa mahakamani humo kwamba, Februari mwaka jana, washtakiwa hao kwa pamoja walitekeleza mauaji hayo ya Patricia na kuufukia mwili wake kwenye shimo jirani na nyumba yake katika Kijiji cha Rau-Mrukuti Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro na kuficha ukweli huo kwa zaidi ya miezi 10.

Inaelezwa kuwa washtakiwa hao kwa pamoja walikuwa wakimtibu marehemu aliyekuwa mgonjwa.

Wakati matibabu hayo yakiendelea, inadaiwa kuwa tayari walikuwa wametumia fedha za mama yake zaidi ya Sh. milioni 60.



Mafundi wakikarabati uzio wa kituo cha mabasi ya mwendokasi cha Kimara Mwisho, Barabara ya Morogoro, Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam jana, ambacho baadhi ya maeneo yameharibika kwa kugongwa na magari. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Nape asema hakuna wizi vifurushi vya simu

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema hakuna wizi wa vifurushi katika mitandao ya simu huku ikibainisha kuwa wamejiridhisha kuwa hakuna kitu kama hicho baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa watu mbalimbali, wakiwamo viongozi.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alitoa kauli hiyo jana wakati akihojiwa katika kipindi cha 'Power Breakfast On Saturday' kinachoendeshwa na Clouds FM na Clouds TV baada ya wananchi kuendelea kulalamikia suala hilo.

Miezi kadhaa iliyopita kuliibuka madai kwamba kuna wizi katika vifurushi vya mitandao ya simu za mkononi, hivyo Waziri Nape akawataka wale wanaoamini kwamba wanaibiwa kwa kukuta vifurushi vimeisha bila kukitumia, wapeleke ushahidi ili ufanyiwe uchambuzi kwa kutumia vifaa vya kisasa na kuwekwa hadharani.

Akizungumzia mwitiko baada ya wito alioutoa awali, Nape alisema walijitokeza wengi wakiwamo viongozi (bila kuwataja) lakini baada ya kufanyiwa tathmini, walibaini tatizo lilipo.

"Kinachokujibu si mtu ambaye atasema huyu ni Nape nimbanie hivi. Ni mitambo ambayo imewekwa na mamlaka na watoa huduma wanapitia kuona kama mitambo inadanganya.

"Kile unachopewa ni kile ulichokinunua, bando linaishaje? Hii ndiyo changamoto bahati nzuri tangu nimeanza kulizungumza hili jambo nilitoa ofa kwamba kama kuna mtu anaamini ameibiwa aje atusaidie kupata ushahidi wa huo wizi," alisema.

Waziri Nape alisema wako watu wengi ambao walijitokeza na wanapokwenda na kufanyiwa tathmini wanaondoka hawarudi hadharani.

"Waliojitokeza ninao wengi sana na wengine ni viongozi kabisa anakuja anasema 'Waziri bwana...' ninamwambia kaa hapa, anasema 'bwana mimi nilinunua hiki (kifurushi) angalia imefika hapa hata muda haujafika, kimeisha' wanachukua simu wanaweka kwenye mtandao ninamwambia angalia MB zako zilivyokwenda .

"Ninamwambia hapa ulifanya hii kazi ukaiacha ikaendelea nyuma ya pazi, kwa sababu hii simu hata ulivyoifunga hivi, kuna mambo yanaendelea nyuma ya pazia na mengi yanakula data," alisema.

Alisema baada ya watu hao kuonyeshwa hilo hushauriwa wazime baadhi ya vitu kisha wanunue kifurushi kile kile cha awali na kuona mabadiliko ya matumizi.

Kutokana na hilo, waziri aliwataka wateja wa mitandao kuwa makini na simu janja (smartphone) kwa sababu nyingi huwapa machaguo ambayo mtumiaji hasomi maelezo yake kwa kina na kujikuta amechagua huduma inayokula kifurushi chake.

"Kwa mfano App ya WhatsApp, kuna vitu vinaendelea huko nyuma ya pazia ambavyo wewe kwa kukubali tu kuwa na App ya WhatsApp, kuna chaguo linakwambia hii App unataka iendelee kufanya kazi au ifanye kazi tu ukiwa unataka kuitumia, watu wengi hawasomi, ukiona hivyo wewe unajibu ok (ndiyo).

"Kinachotokea unakubali vitu vingi vinaendelea bila wewe kujua halafu ukiweka GB tano zinakatika unasema nimetapeliwa," alisema.

Waziri Nape alisema baada ya tathmini hiyo hajapata kesi ya mtu yoyote anayelalamika kwamba hajatendewa haki.

Hata hivyo, waziri huyo alisema serikali haipuuzi na haitapuuza malalamiko ya wananchi kuhusu vifurushi.

Pia alisema bei ya kifurushi cha mwezi na kile cha kila siku masharti yake ni tofauti ambapo cha siku kisipotumika kinaweza kutumika baadaye wakati cha mwezi muda wake ukiisha na chenyewe huisha.

Alisema Sheria za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) haimruhusu mtoa huduma kupandisha huduma bila kupeleka kwanza kwao na huwa kuna mchakato na akiruhusiwa ni lazima autaarifu umma.

Alisema kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa na taasisi za kimataife, Tanzania inashika nafasi ya sita kwa Bara la Afrika kwa kuwa na gharama za chini za vifurushi na nafasi ya 32 duniani kwa gharama ya chini ya data.

Alisema serikali kupitia TCRA imeendelea kufanya tathmini ya gharama za uwekezaji, utunzaji na usafirishaji wa data kila baada ya miaka minne na tathmini nyingine inafanyika mwaka huu ili kupata uhalisia wa gharama za vifurushi kama zitapanda au kushuka.

Nape ameitaka TCRA na kampuni za simu waendelee kuelimisha Watanzania na kujibu maswali yanayoulizwa na wateja nao watumie lugha zenye staha wakati wanahoji huduma.

# Kigogo aliyelalamikiwa asimamishwa kazi

**Na Beatrice Shayo,** TABORA

SERIKALI imemsimamisha kazi Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani Tabora, Absalom Cheliga, kupisha uchunguzi wa tuhuma zinazomkabili na kutakiwa kukabidhi ofisi kwa Jarufu Magubiko.

Juzi, Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alipokuwa katika ziara yake katika wilaya ya Uyui, alipokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa mrajis huyo amekuwa mrasimu na anawakwamisha.

Shaka alishauri kuondolewa kwa mrajis huyo kutokana na kulalamikiwa na wananchi kila wilaya aliyofika akituhumiwa kufanya urasimu na kuwakwamisha wakulima wa tumbaku.

Nipashe ilipata nakala ya barua aliyoandikiwa Cheliga na kutiwa saini na Mrajis wa Vyama vya Ushirika Tanzania, Dk. Benson Ndiege, ikiwa na kichwa cha habari 'Kupumzishwa Kutekeleza Majukumu ya Kazi'.

"Nachukua fursa hii kukujulisha kuwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika imepata malalamiko kutoka kwa viongozi mbalimbali wa chama tawala na serikali pamoja na wadau mbalimbali wa ushirika wakilalamikia utendaji wako unaohusishwa na ukiukwaji wa sheria, kanuni, taratibu na maadili katika utumishi wa umma.

"Kwa kuzingatia malalamiko hayo yanahusisha utendaji kazi, ninakupumzisha kutekeleza majukumu yako ya kazi kuanzia tarehe ya barua hii ili kupisha uchunguzi. Uamuzi huu nimeufanya kwa mujibu wa kanuni 37 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003," alieleza sehemu ya barua hiyo.

Kwa mujibu wa barua hiyo, wakati wa kipindi cha kupumzishwa majukumu yake, haruhusiwi kutoka nje ya kituo chake cha kazi bila idhini ya Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

"Tafadhali andaa hati ya makabidhiano na kabidhi kazi zako kwa Jarufu Magubiko ambaye atasimamia ofisi ya Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika kwa mkoa mpaka hapo maamuzi (uamuzi) mengine (mwingine) yatakapofanyika (utakapofanyika)," ilimalizia barua hiyo.

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 90 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late: HARRIS CHRISTOPHER GARDIAS**

**BY 1. EVAN HARRIS GARDIAS**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the **26 day of AUGUST.........2022**

**Dated at MOROGO this 19 day of AUGUST.........2022**



**RESIDENT MAGISTRATE**

## Mwanafunzi ajinyonga kisa kuungua kwa sare za shule

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MWANAFUNZI wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Maleutsi wilayani Makete, Marko Sanga (12) amekutwa amejinyonga kwa kutumia mnyororo wa baiskeli katika kijiji cha Maleutsi, mji mdogo wa Iwawa.

Mama mkubwa wa marehemu, Obina Mbilinyi, alisema tukio hilo lilitokea Agosti 18, mwaka huu, majira ya saa 9:00.

Alisema chanjo cha kuchukua uamuzi huo ni baada ya mtoto huyo kutoka kufungua ng'ombe shambani na aliporudi nyumbani, akakuta redio aliyokuwa ameiweka chumbani kwake pamoja na sare za shule, vimeungua.

"Kitendo cha kuunguza vifaa vyake zikiwamo nguo, nadhani ndicho kimemfanya achukue uamuzi huo mgumu," alisema Mbilinyi huku akisema hawajawahi kusikia tabia za matukio yasiyoridhisha kutoka kwa mtoto huyo.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Maleutsi, Teruka Mahenge, alisema Sanga alikuwa mwanafunzi mtulivu na maendeleo yake darasani yalikuwa si ya kuleta shaka wakati wote, hivyo wamepata pigo kubwa kwa walimu na wanafunzi wenzake.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Maletsi, Eliudi Sanga, alisema walipokea taarifa majira ya saa tisa za tukio la kujinyonga kwa mtoto huyo na kwamba ni jambo la kwanza kutokea na limeleta taharuki katika eneo hilo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamis Issah, amethibisha kutokea kwa tukio hilo na kuwataka wazazi kuishi vizuri na watoto na kuwalea katika maadili mazuri.

"Ndani ya kipindi hiki cha likizo tukio hili ni la pili kwa mtoto kujitoa uhai, hivyo kuna haja ya wazazi kuwa karibu na watoto hasa katika suala la malezi ili kukabiliana na matukio ya aina hii," alisema Kamanda Issah.



Viongozi wa Kata ya Makojo na wadau wa afya wakiwa katika ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa kituo cha afya cha kata hiyo, wilayani Musoma mkoani Mara juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Simulizi machungu aliyepata ajali gari miaka 20 iliyopita

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HUJAFA hujaumbika. Ndivyo unavyoweza kuelezwa kutokana na mateso na machungu anayopitia Magreth Mwibule (42) (pichani) mkazi wa Bahi Road jijini Dodoma, kutokana na ajali ya gari aliyoipata miaka 20 iliyopita.

Pamoja na maumivu anayopitia, hana msaada, chakula chake ni bahati nasibu huku ndugu zake wakiwa wamemsusa na sasa anahudumiwa na watoto wake wa kiume ambao bado ni wadogo na wanafunzi.

Kutokana na hali hiyo, amewaomba wasamaria wema na serikali kumsaidia kupata matibabu ya uti wa mgongo ambao umesababisha kulala kitandani kwa takribani miaka 10.

Akizungumza na Nipashe juzi nyumbani kwake, Mwibule alisema chanzo cha tatizo hilo ni ajali mbaya ya gari aliyoipata ambayo ilimsababishia fuvu la mbele ya kichwa kutolewa.

Mama huyo wa watoto wawili, alisema alipata ajali hiyo mwaka 2002, akiwa amehitimu kidato cha nne, iliyosababisha na kushindwa kutimiza ndoto zake kielimu na kimaisha.

"Ajali niliyoipata niliipata siku moja na ile ajali kubwa ya treni iliyoua hapa Dodoma. Nilitibiwa kama mmoja wa majeruhi wa ajali ya treni. Namshukuru Mungu madaktari walipambana kuokoa uhai wangu. Hapa kwenye fuvu la mbele mifupa ilitolewa kabisa ndiyo maana unaona nina hali hii," alisema.

Kutokana na hali hiyo, alisema haikubainika mapema kuwepo kwa tatizo la pingili kwenye uti wa mgongo hadi ilipopita miaka kadhaa na kuanza kuugua ghafla huku akishindwa kusimama.

"Mwaka 2011 nilianza kusikia maumivu makali na yalizidi kupanda siku hadi hadi siku jambo lililosababisha kushindwa kabisa kufanya kazi yoyote na hadi sasa nipo kitandani," alisema.

Mwibule alibainisha kuwa mume wake alimuoa akiwa na tatizo hilo na alifariki dunia mwaka 2010 na kumwachia watoto hao huku familia ikimtelekeza bila kumpa msaada wa aina yoyote. Alisema anapitia kwenye maumivu makali ya uti wa mgongo na hana uwezo wa matibabu. Alisema kutokana na ushauri aliopewa na madaktari kwenye hospitali mbalimbali, anatakiwa kutibiwa nje ya nchi ili kurejea kwenye hali yake ya kawaida.

"Kula yangu na wanangu na hata kodi ya pango tunaishi kwa hisani ya wasamaria wema, ambao wanatusaidia lakini na waumini wenzangu. Naomba Watanzania wenzangu mnisaidie nipate matibabu niwe na uwezo hata wa kufanya kazi ndogo za kuhudumia wanangu.

"Napitia maumivu makali, mimi si wa kutoka nje. Hata kwenda chooni najisaidia hapa hapa na nahudumiwa na hawa watoto wangu wa kiume ambao ni wadogo. Mmoja yuko kidato cha tatu mwingine cha kwanza. Hawana jinsi, inabidi wanihangaikie hivyo hivyo.

"Naomba msaada wa matibabu iwe ndani au nje ya nchi kikubwa nipate uponyaji. Kuna msamaria alinipeleka Hospitali ya Benjamin Mkapa, wakaangalia na kunieleza kuwa umri wangu hawawezi nifanyia upasuaji kutibu tatizo langu. Nilipewa dawa tu za kutuliza maumivu, wakashauri kwa nje ya nchi inawezekana lakini hawakuniambia ni nchi gani," alisema.



Kutokana na mateso anayoyapitia, anaomba msaada kutoka kwa wasamaria wema ili apate matibabu na kupunguza maumivu anayopitia lakinipia msaada wa kimaisha yeye na watoto wake ili waendelee na masomo.

Kwa mujibu wa Mwibule, hivi sasa amejistiri na watoto wake kwa msaada wa mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Umonga jijini hapa.

Ameomba kwa wale wenye nia ya kumsaidia kuwasiliana naye kwa namba 0759-233513.

# Shaka aagiza kuvunjwa kwa mkataba ujenzi barabara

**Na Beatrice Shayo,** TABORA

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) Itikadi na Uenezi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, ameagiza kuvunjwa kwa mkataba wa mkandarasi aliyepewa kazi ya kujenga barabara zenye kilometa 39 katika wilaya ya Uyui kwa kushindwa kukidhi viwango na uzembe.

Kampuni ya ujenzi ya Kasco iliingia mkataba na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini (TARURA) kujenga barabara hiyo tangu Novemba, mwaka jana, kwa gharama ya Sh. milioni 499 na mpaka sasa imetumia Sh. milioni 60.

Shaka alitoa ushauri huo jana wakati akizungumza na wananchi wa kata ya Igulungu baada ya kukagua ujenzi wa shule ya sekondari wilayani Uyui nakupokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu ubovu wa barabara hali inayowasababisha wajawazito kujifungulia njiani.

Shaka alisema ni jambo la kushangaza fedha imetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara na mkandarasi anafanya kazi kwa kusuasua huku wananchi wakiendelea kuteseka.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amepelekea Sh. milioni 499 tangu Juni, mwaka jana, kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara na mpaka sasa mkandarasi amechukua Sh. milioni 60.

"Mpaka kufikia leo (jana) ni kama mnavyosikia wenzetu wako mbioni, mchakato wa kusitisha mkataba, muda si mrefu, yaani hadithi imekuwa ndiyo hiyo. Mkandarasi uwezo hana atimuliwe haraka sana," alisema Shaka.

Pia Shaka alimtaka Mkuu wa Wilaya ya Uyui, Makore Kisare, kulisimamia jambo hilo kwa kuwa hawawezi kwenda kwa mwendo huo, kila mwananchi anayesimama analalamikia ubovu wa barabara.

"Sisi wenyewe tumekuja tumeona hali ya barabara, kinamama wanalia na Rais wao kwa sababu wakienda kujifungua wanapata changamoto na Rais Samia ameleta fedha. Kuna watu wanakwamisha haikubaliki," alisema Shaka.

Alisema lengo la kuanzishwa kwa TARURA ni kuhakikisha inawasaidia wananchi ujenzi wa miundombinu ya barabara ili kuwarahisishia usafiri kwenye mazao, bidhaa na hata kufuata huduma za kijamii.

Shaka alisema ni muhimu TARURA kuwatumia makandarasi wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi ili kuhakikisha miradi wanayopatiwa inakamilika kwa wakati ikiwa na ubora unaotakiwa.

Meneja wa TARURA Wilaya ya Uyui, Mhandisi Rahabu Thomas, alisema hivi sasa wako katika mchakato wa kufuata sheria za mkataba kwa kuwa tayari wamebaini mkandarasi huyo hana uwezo wa kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo kwa viwango.

Alisema muda wa kukamilisha barabara hizo kwa mujibu wa mkataba ni miezi sita na fedha ipo tangu mwaka jana lakini mkandarasi anasuasua mpaka sasa.

Naye Kisare alisema wakati TARURA inaingia mkataba na mkandarasi Novemba, mwaka jana, baada ya hapo kilifuata kipindi cha mvua na mkandarasi alishindwa kufanya kazi mpaka Mei, mwaka huu, ndipo ameanza kufanya kazi.

Alisema licha ya kushindwa kufanya kazi katika kipindi alichosainishwa mkataba na TARURA kwa sababu za mvua bado ni mzembe.

"Naomba niseme kama ambavyo TARURA imeanza kuchukua hatua, huyu mkandarasi ni mzembe hata ukiangalia ubora wa barabara anayoitengeneza haina viwango," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Ujerumani yaahidi kusaidia ujenzi VETA

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, ameishukuru Ujerumani kwa kuahidi kuendelea kuisaidia Tanzania kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa vyuo vya ufundi (VETA) vitakavyosaidia kukabiliana na tatizo la ajira hususan kwa vijana.

Dk. Nchemba aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipokutana na kufanya mazungumzo na Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo wa Ujerumani, Dk. Barbel Kofler.

Alisema kipaumbele cha serikali ni kujenga vyuo vya ufundi katika wilaya 72 ambazo hazina taasisi hizo za mafunzo, hivyo ili kutatua tatizo la ajira linalowakabili wananchi na kuiomba Ujerumani kusaidia ujenzi wa miundombinu ya vyuo hivyo pamoja na zana za kufundishia na kujifunzia.

"Eneo ambalo tumelizungumzia linaenda sambamba na mwelekezo wa Rais Samia Suluhu Hassan ni ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi (VETA) katika wilaya ambazo hazina vyuo ili kuwaandaa vijana kukabiliana na ukosefu wa ajira," alisema Dk. Nchemba.

Dk. Nchemba alimshukuru mgeni wake kwa utayari wa serikali yake wa kusaidia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii ambayo nchi hiyo imekuwa ikishirikiana na Tanzania ikiwamo ya afya, elimu, hifadhi ya mazingira na utalii.

Kuhusu usawa wa kijinsia na udhibiti wa vitendo vya ukatili wa kijinsia, Dk. Nchemba, alimhakikishia Naibu Waziri huyo kwamba serikali imepiga hatua kubwa katika kukabiliana na masuala hayo.

Alisema uwakilishi wa wanawake katika vyombo ya uamuzi umeongezeka na hatua madhubuti zinachukuliwa kukabiliana na vitengo vya ukatili wa kijinsia pamoja na kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, aliipongeza Ujerumani kwa kuendelea kushirikiana na Tanzania kwa kuwa hivi karibuni nchi hizo mbili zilitiliana saini mikataba mitatu yenye thamani ya Euro milioni 45 sawa na Sh. bilioni 119.2 kwa ajili ya kutekeleza miradi mitatu katika sekta za maji, afya na kuendeleza sekta ya maliasili na utalii.

"Tanzania imenufaika na misaada kutoka Ujerumani katika maeneo mbalimbali yakiwamo maji, nishati, matumizi endelevu ya maliasili na utunzaji wa mazingira pamoja na usimamizi bora wa fedha za umma," alisema Tutuba.

Dk. Kofler kwa upande wake alipongeza serikali kwa jitihada mbalimbali wanazozifanya za kukuza uchumi, kuimarisha demokrasia na kuimarisha afya ya jamii na kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana.

Alisema kuwa nchi yake iko tayari kuendeleza ushirikiano na Tanzania katika nyanja mbalimbali za maendeleo ikiwamo ujenzi wa vyuo vya ufundi ambavyo alisema ni muhimu katika maendeleo ya nchi na kwamba uwekezaji unaofanywa na mashirika na taasisi mbalimbali nchini unahitaji nguvu kazi yenye ujuzi.



Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni inayozalisha gesi ya Oksijeni na ya viwandani ya TOL Gases Ltd, Michael Shirima (katikati), akijadiliana jambo na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Daniel Warungu (kulia), katika mkutano mkuu wa wanahisa wa TOL, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kujadili mafanikio. Kushoto ni Wakili Collineries Kiliwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri ataka jumuiya imara kwa mustakabali wa China na Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa China, Wang Yi (pichani), ameshauri kujengwa kwa jumuiya ya China na Afrika yenye mustakabali wa pamoja katika enzi mpya.

Wang alitoa pendekezo hilo Alhamisi wiki hii katika mkutano wa kukagua maendeleo yaliyopatikana katika ushirikiano kati ya China na Afrika.

Novemba, mwaka jana, Mkutano wa Nane wa Mawaziri wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika (FOCAC) ulifanyika Dakar, Senegal na China ilitangaza kutekeleza programu tisa kwa pamoja na nchi za Afrika, ikiwa kuonyesha dhamira yake ya kuendelea kwa Afrika na kasi endelevu ya ushirikiano wa pande hizo.

Taarifa ya Shirika la habari la China (Xinhua) ilisema katika mkutano wa Alhamisi wa waratibu kuhusu utekelezaji wa matokeo ya mkutano wa Dakar, uliofanyika kwa njia ya mtandao, Wang alisema China na Afrika zimetekeleza kwa pamoja matokeo hayo kwa maendeleo mazuri na kuleta manufaa yanayoonekana kwa watu wa Afrika.

"China na Afrika zimefanya kazi kwa dhati ili kulinda haki ya kimataifa, kusukuma ujenzi wa miundombinu ili kuwezesha harakati za ukuaji wa viwanda barani Afrika, kukabiliana kwa pamoja na tatizo la chakula duniani na janga la UVIKO-19, kutafuta maendeleo endelevu kupitia ushirikiano wa nishati safi na mabadiliko ya majibu ya mabadiliko ya hali ya hewa pamoja na kukuza amani na utulivu wa kikanda," alisema Wang.

Alibainisha kuwa mwaka huu ni kumbukumbu ya miaka 20 tangu kuanzishwa kwa Umoja wa Afrika (AU), hivyo Wang alisema China na Afrika zinapaswa kuungana kwa kariibu zaidi kutafuta maendeleo na ukuaji wa pamoja na kujenga kwa dhati jumuiya yenye mustakabali wa pamoja katika enzi mpya.

Ili kufikia hatua hiyo ya kimaendeleo, alipendekeza mambo matano la kwanza likiwa kwa pande zote kushikilia kanuni ya uaminifu, matokeo halisi, upendo na imani nzuri, na kuimarisha umoja na kusaidiana.

Katika suala hilo, alisema China iko tayari kufanya kazi na Afrika kuendeleza misingi mitano ya kuishi kwa amani, kutekeleza mfumo wa kweli wa pande nyingi na kulinda kwa pamoja haki na maslahi halali ya nchi zinazoendelea.

Pili, alisama China na Afrika zinapaswa kujitolea kwa maendeleo ya pamoja na kwamba China itaendelea kuchukua jukumu kubwa katika ujenzi wa miundombinu mikubwa ya Afrika, kuendelea kuongeza uingizaji bidhaa kutoka Afrika, kuunga mkono ukuaji wa viwanda vya kilimo na viwanda vya Afrika na kupanua ushirikiano katika viwanda vinavyoibukia.

Pendekezo la tatu ni pande zote mbili kujitolea kwa uhuru na kukuza kwa pamoja amani ya kikanda. Alisema China itaendelea kuunga mkono suluhu za Afrika kwa masuala ya Afrika, kupinga uingiliaji wa nje katika masuala ya ndani ya nchi za Afrika na kupinga kuanzisha makabiliano na migogoro barani Afrika.

Jambo la nne, alisema China na Afrika zinapaswa kudumisha urafiki wa jadi na kukuza mabadilishano kati ya watu na watu huku akibainisha kuwa China iko tayari kukabiliana na matatizo yanayosababishwa na janga hili na kuwasaidia wanafunzi wa Kiafrika ambao awali walisoma nchini China kurejea.



Katika jambo la tano, alisema pande zote zinapaswa kuzingatia uwazi na ushirikiano wa ushindi pande zote ili kukuza maendeleo mazuri ya ushirikiano wa kimataifa na Afrika.

Mkutano huo ulihudhuriwa na Aissata Tall Sall, Waziri wa Mambo ya Nje wa Senegal, Mwenyekiti Mwenza wa Afrika wa FOCAC, wawakilishi wa kanda ndogo za Afrika na Kamisheni ya Umoja wa Afrika na wajumbe wa kidiplomasia wa nchi za Afrika nchini China.

Walisisitiza kuzingatia kanuni za haki za kimataifa na kutoingilia mambo ya ndani, kufuata kanuni ya kuwa na China moja na uungaji mkono thabiti wa juhudi za China za kulinda mamlaka ya kitaifa na uaminifu wa eneo.

Upande wa Afrika uko tayari kufanya kazi na China ili kuendelea kuimarisha ujenzi wa mifumo ya kongamano na kuendeleza uboreshaji wa ushirikiano wa Afrika na China, kwa mujibu wa wanadiplomasia hao wa Afrika.

# TCRA yatakiwa kudhibiti uhalifu katika mitandao

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Khalid Salum Mohamed, ameitaka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kuongeza ujuzi wa wataalamu wanaodhibiti matukio ya uhalifu mtandaoni ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia.

Rai hiyo aliitoa jana jijini Dar es Salaam alipofanya ziara TCRA kukagua shughuli zinazofanyika katika kuhakikisha mamlaka hiyo inatoa huduma za viwango vya juu na kudhibiti matukio ya uhalifu. Alisema ameridhishwa kwa kiasi kikubwa na namna mamlaka hiyo inavyofanya kazi tofauti na mtizamo wake wa awali na kuhimiza kuongeza juhudi za kuzuia matukio ya uhalifu mitandaoni.

"Teknolojia inabadilika, hivyo wataalamu wetu wanatakiwa kuwa na ujuzi zaidi wa kudhibiti uhalifu. Unaweza kuona hasara zaidi kuwajengea uwezo lakini hasara kubwa zaidi ikawa katika kudhibiti uhalifu unaotokea ambao ungeweza kudhibitiwa," alisema Mohamed.

Pia aliitaka TCRA kufanya ukaguzi wa kudhibiti hatari katika maeneo yenye minara ya mawasiliano ambayo inakuwa karibu na makazi ya watu na kuongeza juhudi za kuongeza mawasiliano kufikia maeneo yote ambako huduma hiyo haijafika au yenye changamoto za mawasiliano. Mkurugenzi Mkuu wa TRCA, Dk. Jabiri Bakari, alimshukuru waziri huyo kwa ziara yake na kuahidi kuendelea kuongeza ushirikiano wa serikali ya Zanzibar. Alisema TCRA inatoa huduma hadi upande wa Zanzibar na uwapo wake ni kuona ufanyaji kazi wa mamlaka pande zote mbili za muungano na namna ya kuboresha uchumi wa buluu kupitia sekta hiyo.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Tahadhari ichukuliwe taarifa uhaba wa nafaka hasa mahindi

**KATIKA** mikoa mbalimbali nchini, kumesikika kilio cha kuwapo kwa uhaba wa mahindi hasa kutokana na madai ya uwapo wa wafanyabiashara walioingia vijijini na kununua mazao kisha mengine kuyaficha na baadhi kusafirisha nje ya nchi.

Kilio hicho kimesikika katika mikoa ya Mbeya, Ruvuma, Dodoma, Manyara, Arusha na Katavi ambako imedaiwa kuwa kumekuwa na wimbi la wafanyabiashara waliovamia maeneo mbalimbali na kuwashawishi wananchi kuwauzia mazao hayo kwa bei ya juu.

Baadhi ya wafanyabiashara hao wamedaiwa kuwa baada ya kununua wanayaficha kwa lengo la kusubiri bei ipande ili wayauze.

Kutokana na hali hiyo, kuna uwezekano mkubwa wa kuwapo na uhaba mkubwa wa mahindi ambao utasababisha baa la njaa katika maeneo mbalimbali nchini ikizingatiwa kuwa katika msimu wa kilimo mwaka huu, mvua hazikuwa za kutosha hali ambayo ilisababisha mavuno kuwa kidogo.

Hata nchi jirani pia zilikumbwa na hali hiyo, jambo ambalo limesababisha wafanyabiashara kutoka mataifa yanayoizunguka Tanzania kudaiwa kuingia nchini na kununua bidhaa hiyo na ama kusafirisha au kuhifadhi kusubiri kupanda kwa bei.

Kilio hiki kinakuja muda mfupi tangu Rais Samia Suluhu Hassan alipotoa angalizo kwa wananchi waliopata mazao kwa kiasi wakati wa mavuno kuhakikisha wanatumia kwa uangalifu wakati taifa likifanya tathmini ya hali ya upatikanaji wa chakula na akiba iliyopo kabla ya kutoa ruhusa ya kuuza.

Ikiwa haujapita muda, tayari zimesikika taarifa za kuadimika kwa nafaka hasa mahindi, hivyo kuashiria hatari ya kuwapo baa la njaa na hata kwenye maeneo yatakakopatikana kuuzwa kwa bei ya kuruka.

Kuwapo kwa bei ya juu kutasababisha wananchi wengi kushindwa kununua kutokana na hali zao za kipato na matokeo yake wataingia kwenye adha kubwa ya ukosefu wa chakula.

Wahenga wanasema tahadhari kabla ya hatari. Kwa msemo huo, tahadhari kubwa inapaswa kuchukuliwa na viongozi katika ngazi mbalimbali ili kuhakikisha, kwanza, agizo la Rais kuhusu udhibiti wa biashara huria kwa sasa na pili, kudhibiti magendo yanayoendelea ikiwamo kuzuia usafirishaji wa mahindi na nafaka zingine nje ya nchi kabla ya tathmini ya serikali kuhusu upatikanaji wa chakula kutolewa.


Ifahamike kwamba kama alivyosema Rais Samia serikali haijazuia biashara ya nafaka na usafirishaji kwenda nje bali kinachotakiwa ni kuangalia hali halisi kabla ya kufunguliwa milango. Kwa mantiki hiyo, wananchi waliobahatika kupata mavuno kiasi, wawe wastahimilivu ili serikali ijiridhishe na uhakika wa akiba ya chakula.

Pamoja na hayo, kabla ya kuuza kwa wafanyabiashara kutoka nje, kama alivyoshauri Rais, ni vyema wakulima wakatoa kipaumbele kwa kuuzia Wakala wa Taifa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kwa kuwa kufanya hivyo kutaongeza uhakika wa chakula kwani hata kikikosekana mikononi mwa wananchi, kitapatikana humu humu nchini.

Ili kuhakikisha jambo hilo linafanikiwa, ni vyema viongozi wa serikali katika ngazi mbalimbali wakachukua hatua za kuwaelimisha wananchi pamoja na kuzuia biashara hiyo kwa muda kama ilivyoagizwa na mamlaka za juu.

Hakika kusifanyike mzaha katika suala hilo kwani kama suala hili litaachwa kama lilivyo, kuna hatari kubwa ya kuwapo baa la njaa na maafa miongoni mwa wananchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

## Hongera serikali kujenga kituo matibabu saratani

Na Adam Fungamwango

**NI** ukweli usiopingika kuwa ugonjwa wa saratani nchini umekuwa ukiongezeka siku hadi siku kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo mtindo wa maisha na vyakula vya kisasa.

Wala siyo siri miaka ya nyuma, ukisikia mgonjwa wa saratani basi ni wale wenye uwezo mkubwa wa kifedha, au wenye mamlaka na nyadhifa mbalimbali. Kifupi ni wafanyabiashra wakubwa na vigogo na haukuwa ugonjwa ambao unawapata watu wenye hali ya chini.

Yeyote atakayesikia mtu amepatwa ugonjwa wa saratani, au amefariki kwa ugonjwa huo, huyo mtu anatakuwa mtu mzito. Ni kwa sababu watu wa hali ya chini walikuwa na aina yake ya maisha na vyakula vyao, huku wakubwa nao wakiwa na aina yao ya maisha ya vyakula vyao.

Kwa sasa ni kama watu wote wanafanana tu. Hakuna tofauti kubwa ya maisha na aina ya vyakula. Hata watu wa chini kwa sasa wanakula vyakula vya kwenye makopo, na mtindo wa maisha umekuwa ukifanana sana.

Kutokana na ongezeko la wagonjwa, serikali imekaa chini na kuamua kukubali kituo cha kisasa cha kutoa huduma za uchunguzi kwa wagonjwa wa saratani kujengwa. Kizuri zaidi ni kwamba kituo hicho kitakuwa na uwezo wa kugundua tatizo hilo katika hatua za awali.

Mkataba huo wa ujenzi ulisainiwa juzi kwenye ubalozi wa India nchini, ukihusisha Hospitali ya Apollo na Kampuni ya Eclipse Group Africa ya Dar es Salaam.

Watu mbalimbali walishuhudia utiaji saini akiwamo Balozi wa India nchini Tanzania, Binaya Pradhan na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Afya na Ustawi wa Familia wa India, Lav Agarwal.

Tunaipongeza Serikali ya India, pamoja na ya Tanzania kwa kuwezesha kujenjwa kituo hicho.

Ni ukweli usiopingika kuwa mara nyingi wagonjwa wa saratani nchini Tanzania kuja kugundua tatizo hilo dakika za mwisho.

Wataalamu wanasema kama saratani itagundulika kwenye hatua za mwanzo ni rahisi kupona, lakini kama ikiingia kwenye hatua zinazofuata inakuwa ni ngumu.

Kituo hicho kikikamilika kitawafanya Watanzania sasa kuwa na uwezo wa kwenda kucheki afya zao, hasa kwenye aina hiyo ya ugonjwa ambayo mara nyingi imekuwa ikigundulika kwenye hatua ambayo mgonjwa tayari anaugua.

Huko mitaani mara nyingi wagonjwa wengi wa saratani hasa ya kwenye mapafu, huanza kwa kutapika damu, wengi wamekuwa wakidhani ni kifua kikuu, au wamerogwa, lakini kumbe ni dalili za awali za saratani.

Kama nilivyosema, ugonjwa huu umekuwa na gharama kubwa, huku kukiwa na ongezeko wa wagonjwa ambao ni masikini, hivyo kujengwa na kituo hicho kutasaidia watu kujua afya zao.

Kama walivyosema kituo hicho kitakapomalizika kitahudumia wagonjwa wote wa nchi za Afrika na si Tanzania tu, na kupunguza gharama za wagonjwa kusafirishwa kwenda nchini India.

Kwa hili inapunguza familia za Watanzania kuanza kutafutana na kuanzisha michango kwao, ndugu na jamaa kwa ajili ya kumsafirisha mgonjwa kwenye India, na wakati mwingine mgonjwa anakufa kabla hata michango haijatimia kwa sababu ya kutoanza matibabu kwa wakati.

Kitakapoisha hakutokuwa na mlolongo tena wa kuchanga pesa za matibabu, nauli kwa mgonjwa na atakwenda naye, visa, wakati mwingine mpaka pasipoti, badala yake ni pesa ndogo tu ya matibabu.

Na hata wale wa nchi zingine Afrika, hawatolazimika kusafirisha wagonjwa wao kuvuka bara, badala yake kuwaleta Tanzania wakitumia gharama nafuu, pesa ambazo zitaendelea kuipatia nchi mapato.

Kwa hili serikali ya Tanzania, India zinastahili pongezi na ni mfano wa kuigwa. Pia ni habari nzuri kwa wagonjwa wa saratani ambao wengi wao wamekuwa wakisumbuka bila mafanikio.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Kazi ni moja tu, kuhesabiwa



Na Pascal Mayalla

SERIKALI imepanga Sensa ya Watu na Makazi kufanyika keshokutwa (Agosti 23) ikiwa ni miaka 10 baada ya sensa iliyopita kufanyika. Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar (OCGS) ndio waandalizi, waendeshaji na wasimamizi wa sensa hii.

Kutokana na maandalizi pamoja na hamasa zilizofanyika kutoka kwa viongozi wa serikali, dini na taasisi mbalimbali huku vyombo vya habari vikishinikiza, ni matumaini yangu kwamba maandalizi yote yamekamilika kwa asilimia 100. Kwa maana hiyo, kitu kilichobaki ni kitu kimoja tu, kujitokeza kwa wingi kuhesabiwa.

Sensa ya watu na makazi ni utaratibu wa kukusanya, kuchambua, kutathmini, kuchapisha na kusambaza takwimu za kidemographia, kiuchumi na kijamii kuhusiana na watu wote na makazi yao katika nchi kwa kipindi maalum.

Kwa maana nyingine, sensa ni jambo maalum lenye lengo la kupata idadi ya watu wote katika nchi, kwa umri na jinsia, mahali wanapoishi na hali yao ya elimu, ajira, vizazi na vifo na hali ya makazi. Takwimu hizi za msingi ndizo zinazoweza kuainisha mahitaji halisi ya wananchi yakiwamo makundi maalum yenye uhitaji maalum kwa mfano, watu wenye ulemavu, wanawake, watoto, vijana na wazee hivyo kurahisisha uandaaji wa sera na mipango ya maendeleo kulingana na uhitaji na mazingira yaliyoko.

**Umuhimu wa kipekee wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 ni pamoja na:-**

- Kuisadia serikali kupata taarifa za msingi zitakazosaidia mchakato wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025, mageuzi ya masuala ya afya na jamii na ufuatiliaji wa ajenda za maendeleo za kimataifa.
- Taarifa za idadi ya watu husaidia katika mamlaka za wilaya katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ambayo huakisi matakwa ya watu katika ngazi husika na kusaidia kwenye uwiano wa mgawanyo wa rasilimali;
- Taarifa za msingi za hali ya kidemografia, kijamii na kiuchumi za idadi ya watu na makazi za mipango katika ngazi zote;
- Kigawio katika kukokotoa viashiria vingine mfano pato la mtu mmoja mmoja, pato la taifa, ajira na ukosefu wa ajira na kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi;
- Taarifa itakayowezesha serikali kujua ongezeko la idadi ya watu, kwa mgawanyo na viashiria vingine, ambavyo ni muhimu kwa usimamizi wa mazingira na;
- Msingi wa utawala bora na ujumuishaji wa demokrasia.

Takwimu sahihi za sensa zinahitajika kwa ajili ya ugawaji wa majimbo ya uchaguzi kwa ufanisi, kurekebisha mipaka ya kiutawala katika serikali za mitaa.

Sensa ya mwaka 2022 kama zilivyo sensa zilizopita itatumia aina mbili kuu za madodoso. Dodoso refu litakalotumika kuhoji asilimia 30 ya maeneo yote ya kuhesabia watu na dodoso fupi litakalotumika kuhoji kwenye asilimia 70 ya maeneo yote ya kuhesabia watu.

Madodoso mengine ni dodoso la taasisi ambalo ni mahususi kwa ajili ya wasafiri, waliolala hotelini au nyumba za wageni na waliolazwa hospitalini; na dodoso la wasio na makazi maalum ambalo ni mahsusi kwa watu wote wanaolala maeneo yasiyo rasmi, kwenye mabaraza ya majengo mbalimbali, kwenye madaraja na maeneo mengine.

Kuhusu maswali yatakayoulizwa, Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 ina moduli 14 ambazo zitatumika kukusanya taarifa za watu na makazi yao nchi nzima. Maswali yatakayoulizwa yatahusu taarifa za kidemografia (umri, jinsi, uhusiano, hali ya ndoa, uraia, na kadhalika; maswali yanayohusu ulemavu; taarifa za elimu; maswali ya uhamaji pamoja na taarifa za Watanzania wanaoishi nje ya nchi.

Maswali mengine ni kuhusu umiliki wa nyaraka za kitaifa (vitambulisho vya taifa yaani NIDA, Mzanzibari mkazi, cheti cha kuzaliwa, hati ya kusafiria, na leseni ya udereva); shughuli za kiuchumi; umiliki wa ardhi na taarifa za teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA); na taarifa za uzazi na vifo vilivyotokea ndani ya kaya.

Pia mambo mengine yatakayoulizwa ni vifo vitokanavyo na uzazi; hali ya nyumba za kuishi na umiliki wa rasilimali mbalimbali; maswali ya kilimo na mifugo na mifuko ya hifadhi ya jamii.

Pamoja na kuwapo kwa maswali hayo, ni bahati mbaya kwamba hakuna swali lolote kuhusu idadi ya Watanzania wanaoishi maisha ya kubangaiza, wamachinga au wale wanaendesha maisha yao kwa kuitegemea ile ajira ya kwanza kabisa duniani baada ya binadamu kuumbwa. Hii ni taaluma kongwe inayoongoza kuajiri watu wengi zaidi duniani kuliko ajira nyingine yoyote.

Hata kama serikali yetu haitambui kuwa ni kazi halali, kwa vile ipo na inafanyika na ndiyo imeajiri idadi kubwa kabisa ya watu kuliko ajira nyingine yoyote, kwenye sensa ilibidi tujue ni Watanzania wenzetu wangapi wanaitegemea ajira hiyo kuendesha maisha yao.

Ajira hiyo iko kwa aina tatu. Kwanza, watu wenye bahati zao, hawa wameajiriwa rasmi muda wote wengine kwa kulipiwa mahari na huduma zao kununuliwa kwa bei ya jumla na mteja mmoja kumiliki jumla kwa kuandikisha na kupata hati miliki, au wengine ni kuchukuana tu au kukubaliana lakini huduma hizo zinakuwa kwa mteja mmoja.

Pili, watu wenye bahati zao kumpata mteja mmoja wa kununua jumla, ile uwezo wa mteja huyo mmoja hautoshelezi mahitaji yote ya mhusika hivyo mhusika kujikuta analazimika licha ya kuuza jumla, pia inambidi auze na rejareja kwa kujiiba kufidia nakisi. Tatu, wale wasio na bahati ya kumpata mteja mmoja wa kununua jumla, hivyo kuwajibika kuuza rejareja kwa mteja zaidi ya mmoja na kwa wateja tofauti tofauti. Pia kuna kundi kubwa la watu ambao wana kazi zao lakini bado wanafanya ajira hii kama za muda mfupi au maalumu kujiongezea kipato.

Serikali yetu ilipaswa ijue takwimu za idadi ya hawa watu wate, wale wenye bahati walioajiriwa rasmi muda mrefu, ndio pekee takwimu zao zitakusanywa na wengine wote hazikusanywi. Laiti serikali ingekusanya ikajua tu idadi, na si lazima kuirasimisha biashara hii lakini ingejulikana ili tujijue tuna hali gani na kama ni watu hawa wasaidiwe, wajulikane wasaidiwe.

Mimi na familia yangu tutahesabiwa, vipi wewe msomaji wangu?

**Nawatakia Sensa Njema**
**Paskali +255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Keshokutwa msijitokeze, ila mjiandae kuhesabiwa



Na Joseph Kulangwa

SENSA ni hesabu za watu na vitu, ukisema vitu ingiza wanyama na hata majengo na hufanyika baada ya kipindi fulani kirefu, kati ya miaka mitano na 10, inategemea.

Sisi Watanzania hufanya sensa kila baada ya miaka 10, hivyo basi ya mwisho tuliifanya mwaka 2012. Mliokuwa mmekua mnakumbuka mlivyohojiwa nyakati hizo na makarani.

Huwa kuna maandalizi ambayo hutangulia siku yenyewe ili kuwakumbusha tu watu kuwa tunatakiwa kuhesabiwa ili kuisaidia serikali iliyopo kujua idadi ya watu, kwa maana kuna vinywa vingapi vya kulisha, miili mingapi ya kuvika na kulaza.

Safari hii uhamasishaji haukuwa wa kitoto, mpaka nimeshangaa mwenyewe na kujiuliza mbona mwaka 2012 mambo hayakuwa hivi? Jirani yangu akanisoma na kunijibu kabla sijamuuliza, kuwa kila zama na kitabu chake.

Tumefanya uhamasishaji mpaka kukaribia kupotosha, kwa kutumia misamiati mingine ambayo ndugu zetu walioweka makazi katika baadhi ya vijiji wakawa wanashangaa kulikoni!

Hivi katika jambo muhimu kama hili, kulikuwa na sababu ya kuwambia watu eti SENSABIKA kweli? Kwa nini hatukutaka kubaki na kauli mbiu yetu ya Jiandae Kuhesabiwa? Humo humo wengine wakawa wanasema jitokezeni kuhesabiwa!

Hiyo nayo ikataka kupotosha watu wakidhani sensa ni sawa na uchaguzi kwamba kunakuwa na vituo ambako tunakwenda na kadi kama ya mpiga kura unahesabiwa kisha unachovya dole kwenye wino na kuondoka.

Kumbe ndiyo sababu walioanzisha jambo hili wakawa wanasema jiandae kuhesabiwa, kwamba unakaa nyumbani kwako karani anakuja kukuhoji maswali ukiwa kwako na si kutoka, ukitoka tu imekula kwako, hutahesabiwa.

Na ujue usipohesabiwa siku hiyo ina maana utaanza kula chakula nje ya bajeti ya nchi kwa sababu hesabu yako haimo. Lakini la msingi, ni kujua tu kuwa siku hiyo usitoke, utafutwa nyumbani kuhesabiwa hivyo jiandae kuhesabiwa si nenda kahesabiwe. Ukilazimika kutoka acha madaraka kwa mwenzi wako na majibu ya maswali.

Najua yote hayo yalitokana na hamasa za mwaka huu, ambazo kama nilivyosema hapo juu hazikuwa za kitoto. Kama mambo yote yangekuwa yanahamasishwa hivi, nadhani mpaka sasa hakuna mtu ambaye angesalia bila kuchanjwa UVIKO-19!

Hata hivyo, itoshe tu kusema, kuwa siku yenyewe ni keshokutwa, Agosti 23 ambapo hata serikali imeshatangaza kuwa ni siku ya mapumziko kwa walioajiriwa. Hii ina maana kwamba mtapumzika nyumbani mkisubiri kupokea ugeni wa makarani wa sensa.

Hapo hutalazimika kumpa chakula karani labda kwa ukarimu wako tu uliopitiliza au kwa ulafi wa karani kwa sababu serikali imeshamkirimu na yeye yuko hapo na kishikwambi chake alhamdullilahi kukuhoji na umjibu tu maswali anayokuuliza bila kinyongo.

Maswali yenyewe mbona rahisi tu, jina lako, kwa maana utaje matatu, jinsia yako kama ni mwanamume au mwanamke, umri wako na kama umeoa au kuolewa, siku hizi karibu kila mtu ana simu ya mkononi, waambie tu namba yako.

Watataka kujua kama una kitambulisho cha taifa (NIDA) wape tu namba ya kitambulisho chako, shule kama umesoma mpaka darasa la ngapi, usione aibu la nne, la saba, haina shida. Afya yako pia ni muhimu uwaeleze, hata kama ulipata kupumzika Mirembe kidogo huko nyuma, we sema tu haina shida yaliyopita si ndwele.

Shughuli zinazopeleka mkono kinywani ni zipi kama unazo, unamiliki nini na nini kama ni mjengo we wambie, kama ni mkoko sema. Ndiyo sababu ni sensa ya watu na makazi. Hapana nia mbaya katika hilo, ila kuisaidia serikali kujua mambo ya watu wake na kukujua hata wewe.

Najua makarani wameshapitia mafunzo mbalimbali ya jinsi ya kuhoji madodoso, lakini mwonekano wao wanapoingia majumbani mwa watu, atakayekwenda kinyume cha hapo bila shaka taratibu zipo na wananchi msisite kuchukua hatua ya kutoa taarifa kama mtaona kuna ukiukwaji wowote. Watu wakiingiza usiasa, udini, ukabila kataeni.

Tutakapokuwa tumemaliza kuhesabiwa kwa amani na utulivu kama kawaida yetu na kuiachia serikali ifanye majumuisho yake, na kutujuza tuko wangapi wazee kwa vijana, wanawake kwa wanaume, hapo sasa tutakaa kitako na kuanza kuidai huduma.

Sisi kwa hapo kazi yetu itakuwa imekamilika na kuwa sasa zamu yetu kuipiga sensa serikali kwa kuidai itatufanyia nini, ingawa nasi tuna jukumu la kuifanya kitu. Baada ya hapo sasa tutasubiri hamasa nyingine, kwa sababu nchi hii haishiwagi mambo kwa kweli. Jamani sensa ya watu na makazi ni uti wa mgongo wa maendeleo yetu. Mimi niko tayari je, wewe?

**Alamsiki!**




Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas (wa pili kushoto), akizindua huduma ya Mwalimu Spesho ya Benki ya NMB, mjini Songea, mkoani humo mwishoni mwa wiki. Wengine ni Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololet Mgema (kushoto) na (wa tatu kulia) ni Mkuu wa Idara ya Wateja Binafsi wa Benki ya NMB, Aikansia Muro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC akunwa mpango NMB uwezeshaji walimu

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, amezitaka taasisi za fedha nchini kuunga mkono jitihada za serikali kuwawezesha kiuchumi wananchi wakiwamo walimu na watumishi wa serikali.

Kanali Thomas amezitaka taasisi hizo kuiga mfano wa Benki ya NMB katika kuwawezesha wananchi pamoja na kutoa elimu ya masuala ya fedha hasa kwa wale walioko vijijini.

Aliyasema hayo juzi katika uzinduzi wa kongamano la walimu wa halmashauri za Wilaya ya Songea, Manispaa ya Songea na Madaba lililofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Seminari Kuu ya Peramiho wilayani Songea.

Kanali Thomas alisema kila mwaka NMB imekuwa na utaratibu wa kufanya kongamano la walimu maeneo mbalimbali nchini, hivyo kufurahishwa na utaratibu wa kuwakutanisha wadau na kuwapa maelekezo yatakayowainua kiuchumi. Alisema NMB ni miongoni mwa taasisi za fedha bora nchini na kwamba imefanya jambo jema kuona umuhimu wa kuandaa siku maalum kwa ajili ya walimu ambao ni sehemu ya wadau wakubwa ambao wanahitaji kusaidiwa katika kuboresha maisha yao. "Benki hii ni kubwa hapa nchini yenye mtandao mkubwa wenye matawi 227 na hata mashine za kutolea fedha (ATM) 800 zinazoendelea kutoa huduma, hivyo ni benki yenye wateja wengi kuliko zingine. Benki hii ina zaidi ya wateja milioni nne," alisema.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka walimu kuendelea kuwa wateja katika benki hiyo na kuhimiza uongozi wa NMB kuendelea kuandaa programu nyingi si kwa walimu pekee bali hata kwa watumishi wengine wa serikali ili kuwapatia fursa ya kujua na kuongeza ufahamu na huduma zinazotolewa na taasisi hiyo. Mkuu wa Idara ya Wateja Binafsi wa NMB, Aikansia Muro, alisema benki hiyo imekuwa na mpango maalum kwa ajili ya walimu, maarufu kama 'Mwalimu Special' ambao umejumuisha huduma zote zinazomwezesha mwalimu kupata mikopo yenye riba nafuu ikiwamo ya kujiendeleza kielimu pamoja na watoto, mikopo ya biashara ndogo ndogo, ujenzi na vyombo vya moto.

Pia kupitia mpango huo alisema NMB inawawezesha walimu kupata mkopo wa bima ambayo inawawezesha kulipa bima kujikinga na majanga mbalimbali, mikopo ya pembejeo na mashine za kilimo.Mmoja wa washiriki wa kongamano hilo lilohudhuriwa na zaidi ya walimu 200, Doretha Mbunda, alisema kongamano hilo limewawezesha walimu kuyafahamu mambo mbalimbali ikiwamo kujua namna ya matumizi ya fedha wanapopokea au kupata mishahara na kukumbuka kuweka akiba.

Pia alisema NMB imetoa fursa nyingi kwa walimu kwa ajili ya kuwasaidia katika kuwakwamua kimaisha, kuboresha na kuwawezesha kujiendeleza kielimu pamoja na wategemezi wao.

# Waziri ataka kasi utafiti soko la nyumba kima cha chini

**Na Romana Mallya**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, ametaka mkataba wa makubaliano wa kufanya utafiti kujua mahitaji ya soko la nyumba za kima cha chini utakaowanufaisha Watanzania, kuondokana na changamoto ya makazi utekelezwe haraka.

Ridhiwani aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam baada ya kushuhudia utiwaji saini wa mkataba huo utakaotekelezwa baina ya kampuni ya Tanzania Mortgage Refinance (TMRC) na taasisi isiyo ya kiserikali ya kimataifa ya Habitat for Humanity.

Kiongozi huyo alisema makubaliano hayo yaliyofikiwa yana faida kubwa kwa Watanzania hasa wale wenye kipato cha chini.

"Ukiangalia mkataba huu, Habitat for Humanity wanakwenda kutoa msaada mkubwa kwenye kufanya utafiti kujua mahitaji ya Watanzania, aina ya nyumba zinazohitajika na kujua idadi inayotakiwa. "Kwa sasa tuna watu milioni tatu ambao wanakadiriwa hawana nyumba zilizo bora, kupitia mpango huu kwa kiasi kikubwa hilo linakwenda kufikiwa," alisema.

Ridhiwani alisema juhudi zinazofanywa ni moja ambazo serikali inaziunga mkono kwa kiasi kikubwa kwa sababu malengo yake ni kuhakikisha Watanzania wanaishi katika mazingira mazuri ifikapo mwaka 2025.

Alisema malengo hayo yafikiwe juhudi mbalimbali zinafanyika na wizara hiyo kwa sasa wanatengeneza ramani za kidigitali ambayo inafanyika sanjari na sensa ya watu na makazi inayotarajia kufanyika Agosti 23, mwaka huu.

Pia alisema mpango huo unakwenda sambamba na kuhakikisha watu wa hali ya chini wanatambuliwa.

"Ndani ya sensa pia tunaangalia mazingira wanayoishi Watanzania, tunakwenda kuangalia nyumba walizonazo, hata kama mtu ana kiwanja au ameanzisha msingi tunakwenda kuangalia.

"Ukichukua juhudi hizi za serikali na hii inayofanywa kupitia mkataba huu uliosainiwa leo (jana) unaona Tanzania ya kesho inakwenda kuwa nzuri zaidi kwa sababu watu wa kima cha chini au wanaoishi mazingira magumu kwa upande wa nyumba wanakwenda kujumuishwa kwa maana kuhakikisha mazingira mazuri yanajengwa," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TMRC, Oscar Mgaya, alisema mkataba huo unaanzisha ushirikiano uliolenga kuimarisha muhstakabali wa makazi Tanzania.

Alisema TMRC na Habitat zitashirikiana kuangalia mahitaji ya soko la nyumba za kima cha chini ambacho mpaka sasa hakijafikiwa kwa kiasi kikubwa.

"Kitu cha kwanza kitakachofanyika Habitat watafadhili Dola 100,000 kwa ajili ya utafiti ambao itaangalia mahitaji ya Tanzania, utafiti huo ndiyo utakaotusaidia kuangalia namna ya kuhamasisha rasilimali fedha ya kusaidia mpango huu," alisema.

Makamu wa Rais wa Habitat for Humanity, Maurice Makoloo, alisema wanafanya kazi kwenye nchi 70 duniani na kwa bara la Afrika wapo nchi tisa Tanzania ikiwamo.

Alisema wamesaini makubaliano hayo kuhakikisha kila mwananchi awe na uwezo wa kupata makazi bora stahiki.

"Utaijua nchi nzuri kwa kutazama namna inavyowashughulikia wasiojiweza, lengo letu ni kuhakikisha tunawaangazia wenye kipato cha chini ili waweze kujengewa mazingira wezeshi ya kupata makazi," alisema.

# DC asitisha operesheni kuwakamata wahamiaji

**Na Gurian Adolf,** NKASI

MKUU wa Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa, Peter Lijualikali, ameiagiza Idara ya Uhamiaji wilayani hapa kusitisha operesheni za kuwasaka na kuwakamata wahamiaji haramu kuelekea sensa ya watu na makazi itakayofanyika keshokutwa.

Lijualikali alitoa agizo hilo jana kwa nyakati tofauti alipokuwa kwenye mikutano maalumu kutoa hamasa ya sensa katika kata za Kabwe, Korongwe na Paramawe.

Alitoa agizo hilo baada ya wananchi kulalamika kuwa operesheni zinazofanywa na Uhamiaji zinaweza kuharibu suala hilo ambalo ni muhimu kwa taifa.

Mkuu huyo wa wilaya aliitaka Idara ya Uhamiaji kusitisha kwa muda operesheni hizo ili kutoa nafasi ya kutosha kwa watu wote kushiriki kwenye sensa kwa kuwa kuendelea na operesheni hiyo kunaondoa umakini wa watu kushiriki.

Akizungumza kwenye mkutano katika kata ya Kabwe, mwananchi Juma Alfonce alisema wako tayari kuhesabiwa lakini wasiwasi wao ni operesheni zinazofanywa na Uhamiaji kiasi cha wengi kushindwa kukaa kwenye makazi yao.

"Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, napenda kushauri Idara ya Uhamiaji ingesitisha kwanza operesheni za kuwasaka na kuwakamata wahamiaji katika kipindi hiki ili kupisha sensa ili wananchi watulie majumbani mwao wahesabiwe. Baada ya sensa kupita ndipo waendelee kwani operesheni hii inaondoa utulivu," alisema.

Kutokana na hoja hiyo, Lijualikali aliwataka wananchi kutokuwa na wasiwasi wowote juu ya sensa kwa kuwa serikali lengo lake ni kutaka kujua idadi ya watu na makazi yao na huduma za kijamii zilizoko katika maeneo yao.

Alisema kwa kutambua hayo, serikali itakuwa na uwezo wa kupanga vyema mipango ya maendeleo kwa watu wake.

Lijualikali yuko ziarani kutoa hamasa kutaka kila mwananchi anapata uelewa wa kutosha juu ya sensa ili kujitokeza kuhesabiwa siku itakapofika.

# MAISHA

AGOSTI 21, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 13

**Ukivaa hivi watanasa**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Pangilia chumba chako kivutie



Ukurasa 12

**SHEREHE**




# Ondoa ukavu wa midomo

Ukurasa 14

## WATOTO


### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA









## AMSHA AKILI





## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI





## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
PAA, UMO, KAMBI, JUMBA, BOMANI, JAMBIA

## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Grace na wenzake walikuwa wakioga ufukweni huku wakiangaliwa kwa karibu na wazazi wao.

Wakati wakiendelea kuoga, wazazi wao waliwaita ili waanze safari ya kurudi nyumbani kwao.

Walipotoka Grace alianza kumuuliza mama yake.

**Grace:** Mama mbona yale maji yana chumvi kuna mtu kaweka?

**Mama:** Hapana mwanangu yameumbwa na Mungu yawe vile yalivyo?

**Grace:** Mbona yale tunayokunywa hayana chumvi?

**Mama:** Yale pia yameumbwa yawe vile

**Grace:** Sasa mbona sikuelewi kama itakuwaje yawe tofauti?

**Mama:** Kuna aina mbili za maji, yapo ya chumvi ambayo ni ya bahari na maji baridi yanayopatikana mtoni na ziwani.

**SWALI**

Tunda linalopatikana katika mti wa mkorosho linaitwaje?

# MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



## Waganga wa jadi walivyoua mwelekeo wa maisha yangu-2

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na kisa cha kijana Selestine alivyoyumba kimaisha kwa kudhani waganga wa jadi wangekuwa msaada na kutajirika. Alisaka waganga hadi Kigali nchini Rwanda lakini leo hana chochote.***

Wiki iliyopita nilisimulia yaliyompata rafiki yake waliyeongozana naye kwa mganga lakini naye akaishia masharti magumu yaliyompoteza hata haijulikani alipo. Sasa leo hebu tumsikie Selestine naye yaliyomkuta katika safari yake hiyo ya kusaka maisha ya kitajiri.

Anasema hivi, baada ya mganga huyo kumalizana na rafiki yake huyo, alimwita na kumwambia maneno yafuatayo;- kwamba wewe ni kijana mdogo sana unaongozana na huyu rafiki yako ambaye anakuzidi umri. Nikamjibu ni kweli.

Akaniambia unapotaka kutafuta mali au utajiri yakupasa usiongozane na mtu kwa sababu anaweza kuchukua nyota yako na kumwacha maskini wa kutupwa. Ndipo akaniambia, mimi jinsi nilivyokuona, wewe nyota yako ipo juu kuliko huyo mwenzako na kwenye paji lako la uso nyota yako inaonekana.

Kama unabisha toka nje sasa hivi nenda duka lolote na ulizia chochote mfano suruali, hata kama bei ni kubwa ukitaja kiasi chako atakubali. Hiyo yote inasababishwa na nyota yako.

> **Pia nyota hiyo imegawanyika sehemu mbili, nyingine kuna utawala yaani uongozi. Sasa wewe uliwasahau mababu upande wa baba na inabidi uandike majina matano waliokufa upande wa baba na mama.**

Pia nyota hiyo imegawanyika sehemu mbili, nyingine kuna utawala yaani uongozi. Sasa wewe uliwasahau mababu upande wa baba na inabidi uandike majina matano waliokufa upande wa baba na mama.

Akanipa sharti kwamba nitafute kamba ya mtu aliyojinyongea, kama utaweza kupata hapa Rwanda au ukalete kwenu Tanzania. Hakikisha unaileta na asijue mtu. Kwangu mimi niliona njia rahisi ni kurudi Tanzania kwa sababu mazingira ya kuipata kamba ilikuwa rahisi.

Nikakumbuka jamaa yangu mmoja ambaye rafiki yake aliwahi kujinyonga kwa kamba na kufa. Hivyo nikaona nikimweleza anaweza kunipatia. Na kweli ndivyo ilivyokuwa nikapata kamba hiyo. Siku iliyofuata nikapanda basi kurudi Tanzania. Ikumbukwe nilionywa nisimuage rafiki yangu na wala sikujua alikomweka. Nikaambiwa nisipite mahali popote pale na nyumbani nifike usiku ili nisionane na mtu yoyote.

Nikaenda kuonana na yule jamaa yangu akaniuliza habari za siku nyingi nikamwambia nasaka maisha. Nikamweleza nina shida, nimetokea Rwanda kwa mganga wa kienyeji.

Ameniambia nitafute kamba ya mtu aliyojinyongea. Naomba nitafutie ile ya rafiki aliyojinyongea. Akaniuliza wewe huogopi? Nikamjibu niogope nini, hapa natafuta maisha na mafanikio yangu ndiyo mafanikio yako! Akaniambia ataniletea baadaye.

Hata hivyo, akanitahadharisha kwa kusema yapo mauzauza, maana kubeba kamba hiyo ni sawa na kubeba mtu aliyekufa kwa kujinyonga au unatembea na ile maiti kabisa. Nikamwambia mimi siogopi. Akaniambia sawa, labda umetoka kwa mtaalamu amekukinga na dawa.

Baada ya saa kumi jioni aliniletea na kesho yake nikaanza safari ya kurudi Rwanda kwa yule mganga. Ila njiani nikakutana na misukosuko ifuatayo;- Kwanza nilipofika na kuketi kwenye basi nikaanza kusinzia nikaota ndoto kwamba watu wanakuja na mikuki na kunitishia hadi nikajikuta napiga kelele.

Nikajikuta nakumbuka maneno ya jamaa yangu kwamba nikibeba hiyo kamba. Ni sawa na umebeba maiti. Tulipofika mpakani mwa Tanzania na Rwanda eneo la Rusumo, ikabidi tushuke wote ndani ya basi tuingie ofisi za Uhamiaji tukaguliwe. Sasa mimi nikawaza ile kamba itakuwaje?

Nikaamua kununua mafagio matatu kisha nikayafunga na ile kamba. Nikaingia ofisi za Uhamiaji, ofisa mmoja akaniambia niweke vitu vyangu chini nikaguliwe. Akaniambia wewe umenunua fagio hizi na kuzifunga na kamba yote hii ya nini? Nikamjibu naenda kufunguia mizigo kurudi nayo Tanzania.

Yule askari akaniambia na iwe ni mizigo kweli isiwe ni kwa matumizi mengine. Nikaingiwa na wasiwasi kuwa labda ameshtukia ile kamba. Baadaye tukaingia tena kwenye basi kuendelea na safari kwenda Kigali, Rwanda. Kufika nikaenda moja kwa moja kwa yule mganga.

Kufika mganga akaniambia wewe kweli ni mwanaume kwa sababu nimetimiza sharti ambalo ni gumu. Kisha akachukua mkasi pamoja na ile kamba na kuanza kuikatakata vipande na kuviweka kwenye chungu mfano wa kikaango kisha akatia humo udi. Kisha akanipa karatasi nyeupe na kalamu nyekundu akaniambia niandike majina yangu matatu.

***Mpenzi msomaji, niishie hapa kwa leo. Bado stori inaendelea wiki ijayo. Usikose. Je, una maoni, kisa? Tuma ujumbe mfupi 0715268581.***

# NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



## Sensa ni kwa faida yetu sote, tujitokeze kuhesabiwa

SENSA ya Watu na Makazi hufanyika kila baada ya miaka 10 ili kuiwezesha nchi na serikali kutambua idadi ya watu wake, umri wao, kazi na shughuli za uzalishaji wanazofanya kwa lengo na hatimaye kupata nafasi ya kupanga vizuri mipango ya maendeleo.

Hii ni sensa ya sita kufanyika baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar wa mwaka 1964 uliozaa taifa la Tanzania. Sensa zingine zilifanyika mwaka 1967, 1978, 1988, 2002 na 2012.

Kwa sasa, serikali imetueleza kwamba maandalizi ya sensa ya Agosti 23, mwaka huu, yamefikia asilimia 87 na kwamba kila kitu kinakwenda vizuri kuhakikisha kila Mtanzania anafikiwa na kuhesabiwa.

Sensa ya watu na makazi ni utaratibu wa kukusanya, kuchambua, kutathmini, kuchapisha na kusambaza takwimu za kidemographia, kiuchumi na kijamii kuhusiana na watu wote na makazi yao katika nchi kwa kipindi maalum.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), sensa ni kazi maalum yenye lengo la kupata idadi ya watu wote katika nchi, kwa umri na jinsi, mahali wanapoishi na hali yao ya elimu, hali ya ajira, hali ya vizazi na vifo na hali ya makazi.

Aidha, takwimu hizo za msingi ndiyo zinazoweza kuainisha mahitaji halisi ya wananchi yakiwamo makundi maalum yenye uhitaji maalum kwa mfano, watu wenye ulemavu, wanawake, watoto, vijana na wazee. Kwa kutambua hilo kutarahisisha uandaaji wa sera na mipango ya maendeleo kulingana na uhitaji na mazingira yaliyopo.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), umuhimu wa kipekee wa sensa kwa mwaka huu ni kuisaidia serikali kupata taarifa za msingi zitakazosaidia mchakato wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025, mageuzi ya masuala ya afya na jamii pamoja na ufuatiliaji wa ajenda za maendeleo za kimataifa.

Pia imesema sensa husaidia mamlaka za wilaya katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ambayo huakisi matakwa ya watu katika ngazi husika na kusaidia kwenye uwiano wa mgawanyo wa rasilimali.

Aidha, husaidia kupata taarifa za hali ya kidemografia, kijamii na kiuchumi za idadi ya watu na makazi za mipango katika ngazi zote pia kigawio katika kukokotoa viashiria vingine mfano pato la mtu mmoja mmoja, pato la taifa, ajira na ukosefu wa ajira na kiwango cha uandikishaji wanafunzi.

Aidha, taarifa za mchakato huo zitawezesha serikali kujua ongezeko la idadi ya watu, kwa mgawanyo na viashiria vingine ambavyo ni muhimu kwa usimamizi wa mazingira.

Pia msingi wa utawala bora na ujumuishaji wa demokrasia, kwa kuwa takwimu sahihi za sensa zinahitajika kwa ajili ya ugawaji wa majimbo ya uchaguzi kwa ufanisi, kurekebisha mipaka ya kiutawala katika serikali za mitaa.

Ili sensa ifanyike ni lazima kuna uwekezaji wa fedha kuanzia maandalizi hadi siku yenyewe kwa kuwa watu wataajiriwa kwa muda na watalipwa fedha kwa ajili ya kazi hiyo.

Hizi ni fedha za Watanzania yaani zetu wote tunapaswa kushiriki ili zitumike kwa uhalali na kuleta matokeo tarajiwa kwa manufaa yetu sote. Sensa ya mwisho ilionyesha kuna zaidi ya Watanzania milioni 43.6 na sasa inakadiriwa wako zaidi ya milioni 56. Hata hivyo, kupitia sensa hii, zitapatikana takwimu sahihi.

> **Ni muhimu kila Mtanzania akashiriki kuhesabiwa na kuhamasisha wengine kutoa ushirikiano kwa makarani watakaofanya kazi hiyo kwenye maeneo yao.**

Ni muhimu kila Mtanzania akashiriki kuhesabiwa na kuhamasisha wengine kutoa ushirikiano kwa makarani watakaofanya kazi hiyo kwenye maeneo yao.

Pia ni muhimu watu hususan wa maeneo ya vijijini na pembezo kutambua umuhimu wa sensa, kuacha imani tofauti ambazo siyo sahihi hasa katika kuhesabu watu kwa kuwa hakuna ukweli wowote katika kila wanachoamini bali kwa maendeleo ya nchi.

Kutoshiriki sensa ni kutoshiriki mchakato wa maendeleo yako binafsi na taifa kwa ujumla ni kukwamisha au kuifanya serikali isipate taarifa sahihi za idadi ya watu wake ili inapopanga mipango iwajumuishe kwa ukamilifu wake.

Ni sawa na ndani ya familia baba au mama hununua mlo kulingana na idadi ya wanafamilia, anapoongezeka mwingine maana yake hakuwa kwenye hesabu itakuwa ngumu mlo ulioandaliwa hautatosheleza waliopo, watapunjika.

***Mungu ibariki Tanzania***

## SHEREHE







Katika picha tofauti mtoto Latifa Naseeb maarufu Tiffa, ambaye baba yake Diamond Platnumz ni mwanamuziki nyota nchini akifurahia siku yake ya kuzaliwa.












MITINDO





# Ukivaa hivi watanasa

KUCHAGUA mtindo kila mtu anaongozwa na vigezo binafsi. Lengo kuu la kuongeza ladha kamili katika mwonekano wa mtu.

Bila shaka, mtindo wa mtu haujumuishi mambo ambayo tunapenda, lakini husaidia kuzalisha hisia nzuri ya kuonekana kwako hasa inahusisha mawasiliano na wanawake.

Wanawake wanapenda kuwa na mwanaume mkamilifu amevaa iwe sio kwa gharama kubwa na mpya, lakini inaonekana vizuri.

**Viatu vizuri**

Kwa mujibu wa utafiti wetu, jambo la kwanza wanachoangalia ni viatu vya wanaume. Wanapenda viatu vya sneakers, viatu vya ngozi na simpo.

**Suti kamili ya kiume**

Suti inaweza kuunganishwa kuwa vazi linalopendwa na wanawake kuvaliwa na wanaume zao.

Mwanaume nadhifu wanapenda kuvaa suti, lakini wale ambao wanajua jinsi ya kuchagua.

**Jeans, shati mkali**

Wanawake wengi wanavutiwa na wanaume ambao huchanganya jeans na mashati ya vivuli, pia usisahau kuhusu ubora wa jeans wenyewe.

**Mashati ya mokono mirefu na tai**

Kuonekana kama hivyo unaonyesha kuwa ni mtu mwenye mafanikio kibiashara na ofisini.

Wanawake wanapenda mchanganyiko huo katika nguo.

UREMBO







# Ondoa ukavu midomoni

BAADHI ya watu wamekuwa wakikabiliwa na tatizo la ukavu wa midomo, kitendo ambacho kinawakosesha raha na kuwafanya washindwe kujiamini.

Tatizo hili limekuwa likitokea kwa jinsia zote kwa wanawake na wanaume na mara nyingi umfanye mtu ajihisi kupoteza mvuto.

Sababu zilizotajwa kusababisha hali hiyo ni upepo mkali, ukosefu wa virutubisho mwilini, magonjwa ya ngozi, upungufu wa maji mwilini na baadhi ya vipodozi vyenye kemikali.

Unaweza kutibu tatizo hili kwa kufuata njia zifuatazo.

**Unywaji wa maji**

Kwa kawaida wataalamu wanashauri binadamu anywe maji kulingana na uzito wa mwili wake, lakini ili kufanya midomo yako 'lipsi' kulainika hakikisha unakunywa angalau glasi nane za maji kila siku ili kuboresha ngozi yako.

**Matunda na mboga za majani**

Matunda pia hususani yenye maji maji kama karoti, matango, nyanya na matikiti yanaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa kukinga au kukabiliana na tatizo hili na kuimarisha afya ya ngozi yako kwa ujumla.

**Mafuta ya mgando**

Paka mafuta ya mgando au samli katika midomo yako kila unapotaka kulala, hii itasaidia kufanya midomo yako iwe na unyevunyevu.

**Lipbam**

Hakikisha unatumia mafuta maalum za kupaka katika midomo yako hasa wakati wa baridi 'lipbam'. Majani ya hiliki tumia majani ya hiliki kusugua katika midomo yako hii itakusaidia kuzifanya ziwe laini zaidi.

**Mswaki**

Sugua ngozi ya midomo yako kwa kutumia mswaki na maji ya uvuvugu angalau mara moja kwa wiki, hii itasaidia kuondoa seli zilizokufa katika ngozi ya midomo yako.

**Limao na glycelin**

Paka mchanganyiko wa maji ya limao na 'glycelin' katika ngozi ya midomo yako kila usiku, acha kwa usiku mzima hadi asubuhi ndipo uoshe, hii itakusaidia kung'arisha midomo yako.

**Tui bubu la nazi**

Lainisha ngozi ya midomo yako kwa kupaka tui bubu la nazi katika midomo yako.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Chipsi za viazi vitamu









WENGI tumezoea kupika na kula chipsi za viazi mviringo au mbatata, kuhusu viazi vitamu ni nadra kusikia au kuona mtu akila.

Leo katika safu yetu tutaelekezana namna ya kuviandaa na kupika chipsi zako kwa ajili ya kuliwa na familia.

**MAHITAJI**

Viazi vitamu nusu kilo, wanga wa mahindi vijiko vinne, vijiko vinne vya maji ya baridi na chumvi.

**MAELEKEZO**

Menya na katakata viazi kama chips, osha na kausha viazi kwa kutumia tissues za jikoni. Ukitumia kitambaa kinaweza kubadilika rangi, kuwa mwangalifu.

Changanya wanga wa mahindi na maji kwenye bakuli, ongeza viazi na uchanganye vizuri.

Weka kikaango kwenye moto mkali kiasi, chemsha mafuta hadi yachemke. Weka viazi, usijaze sana kikaango, acha viive kwa nafasi na hakikisha havishikani.

Kaanga mpaka vikaribie kuiva, visipate rangi ya kahawia bado. Toa kwenye mafuta, kausha mafuta kwa kutumia gazeti, mfuko wa karatasi au tishu za jikoni.

Ukimaliza kukaanga na kufuta mafuta yote, zirudishe tena kwenye mafuta kwa kukaanga mara ya pili kwa dakika moja hadi mbili au mpaka ziwe na rangi ya kahawia na zikauke vizuri.

Pakua mafuta yachuje kwenye tishu au chujio la bati, nyunyizia chumvi au viungo vyovyote utakavyopenda.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Namna ya kusafisha feni



NDANI ya nyumba ni muhimu kuweka kipoza joto kama vile feni au kiyoyozi.

Kutokana na vipoza joto kuwa na gharama kubwa, idadi kubwa ya watu wamenunua feni za aina tofauti katika nyumba zao ili kukabiliana na joto.

Ili feni hizo zidumu kwa muda mrefu, zifuatazo ni baadhi ya dondoo za namna ya kusafisha pale zinapokuwa na uchafu.

**1:** Toa nyavu ilifunikwa mbele ya mapanga ya feni.

**2:** Tafuta kitambaa kikavu kidogo na ukikunje kwa ajili ya kufutia.

**3:** Unaweza tumia sabuni ya kusafishia vitu vya plastic au ile ya kawaida ya kufulia.

**4.** Puliza dawa ya kusafishia kwenye mapanga na sehemu nyingine za feni na ufute taratibu na kitambaa

**5.** Baada ya kumaliza kuisafisha rudishia neti yake kama inavyotakiwa.













# Pangilia chumba chako kivutie

SEHEMU au chumba kinachotumika kuvalia nguo (dressing room) ni muhimu na ndiyo mahali pekee ambapo huchangia kumtoa mtu kupendeza au kuchukiza.

Watu wengi wanaokuwa wamependeza wanapotoka ndani na kuvutia machoni mwa watu ikiwamo kusifiwa. Siri yake ni chumba maalum ambacho hutumika kuvalia.

Kutokana na umuhimu huo, leo nataka nizungumzie umuhimu wa kutunza chumba hiki ili kikufanye uwe nadhifu muda wote.

Kuna haja kubwa, kutokana na umuhimu wake, kuhakikisha chumba hiki kinawekwa katika mazingira mazuri ya kuvutia kama ambavyo watu wanaokitumia hutoka humo wakiwa wamependeza na kusifiwa na ndugu, jamaa na marafiki.

Baadhi ya vitu vya kuzingatia katika kuhakikisha chumba chako kinakuwa katika mvuto ni pamoja kupangilia vitu vinavyowekwa kwenye chumba hicho.

Kwa mfano kabati, sitazungumzia kwa ndani vitu vinavyotakiwa kuwa kwenye kabati isipokuwa nataka nionyeshe baadhi tu ya vitu na namna unavyoweza kupangilia.

Katika mpangilio wa kabati unapaswa kuangalia sehemu sahihi ya kuweka kabati lako hilo, liwe la ukutani au kusimama kawaida.

Katika eneo hili, ni muhimu kuwa makini kwa sababu ukifanya makosa kuliweka katika mwelekeo sahihi, kuna hatari kubwa ya kuharibu mwonekano wa chumba chako na hata usifurahie uwapo wa kabati lenyewe na pia likakumalizia nafasi au likawa eneo ambalo halionyeshi mwanga mzuri.


Baada ya kuliweka katika eneo sahihi, tupia macho kwenye eneo lingine tena. Kwa mfano sehemu ya kupangilia mabegi madogo ya mkononi, hakikisha panapangiliwa vizuri. Kama umeyaning'iniza, hakikisha ni yale ambayo yanatumika tu, mengine ambayo huna kazi nayo usiyarundike humo chumbani.

Kadhalika, eneo la kuwekea viatu, nalo lipangilie vizuri. Hakikisha vinavyohifadhiwa chumbani ni visafi.

Kwa ujumla wake, kuweka ubunifu katika mpangilio wa chumba chako ni jambo la muhimu. Kila kitu kilichomo ndani ya nyumba au chumba chako kiwekwe katika utaratibu mzuri. Usiweke vitu vyako ilimradi bali kwa kuzingatia vyote vinatumika kuleta mvuto wa chumba bila kujali ni vya dizaini gani.

Lengo ni kuweka nyumba yako katika hali ya usafi na yenye kuvutia, isiyochosha macho wakati wote, katika kila eneo la nyumba yako.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA 2022
NA MUHIDINI MSAMBA
0656 122770 SMS
...HADUBINI...
AFADHALI UFUMANIWE NA MKE WA MTU KULIKO KUTEMBELEWA NA TAKU-KURU
KASHESHE
SHOGA YANGU NIMEKAA NA SIRI HII MUDA MREFU LEO NIMEONA NIKUELEZE TU NIMEZAA NA MUMEO
HONGERA SANA KWA KUWA MWANAMKE WA HAMSINI KATIKA WANAWAKE WALIO ZAA NA MUME WANGU
KILA NIKIJARIBU KUVUTA TABASAMU HALIJI KABISA KWELI MAISHA SHIKAMOO
UKINITELEKEZA POA TU
LABDA NIPATWE NA KICHAA
NDANI YA KIBASI
KATIKA WATU WANAO JUA SIRI ZETU BASI NI NYIE MNAONGOZA
NA NYIE MNAONGOZA KUTEMBEA NA SISI
BODA BOADA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
... MCHUZI BILA NYANYA NI SUPU..

## Jeshi lafikiria kumruhusu Su Kyi kurejea nyumbani baada hukumu

**YANGON,** MYANMAR

UTAWALA wa kijeshi nchini Myanmar, unafikiria kumruhusu kiongozi aliyeondolewa madarakani Aung San Suu Kyi kwenda katika kifungo cha nyumbani.

Hata hivyo, kutoka kwake gerezani ni baada ya kumalizika kwa msururu wa kesi zinazomkabili.

Taarifa ya kiongozi wa kijeshi, Min Aung Hlaing, iliyosomwa kupitia televisheni ya taifa inafuatia ombi la ofisa mmoja mwandamizi ambaye alitembelea Myanmar wiki hii na kumwomba Suu Kyi kuruhusiwa kurudi nyumbani.

Suu Kyi, aliondolewa madarakani katika mapinduzi ya kijeshi yaliyolaaniwa na wengi mwaka uliopita, mwezi Juni alihamishiwa katika gereza moja la peke yake katika mji wa Naypyitaw.

Tangu mapinduzi hayo, Suu Kyi ameshtakiwa kwa makosa takribani 18, kuanzia ufisadi hadi ukiukwaji wa uchaguzi, na tayari amehukumiwa kifungo cha miaka kadhaa jela.

**DW**

## Nusu ya Watigray wanahitaji chakula

**ADDIS ABABA,** ETHIOPIA

TAKRIBANI nusu ya wakazi wa jimbo la Tigray nchini Ethiopia wanakabiliwa na ukosefu wa chakula.

Hata hivyo, mashirika ya misaada ya kiutu yakihangaika kufikia idadi ya watu kutokana na changamoto ya ukosefu wa nishati ya mafuta, kufuatia mzozo wa hivi karibuni uliodumu kwa miaka miwili.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula linakadiria kuwa viwango vya utapiamlo vimeongezeka na hali inatarajiwa kuwa mbaya zaidi huku watoto chini ya miaka mitano, wajawazito na wanaonyonyesha wakihitaji msaada wa haraka.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani, Tedros Adhanom Ghebreyesus, ambaye anatoka Tigray alisema ubaguzi wa rangi umekuwa ni sababu kwa jumuiya ya kimataifa kutoona hali mbaya wanaopitia watu wa eneo hilo.

Mnamo mwezi Machi serikali ya shirikisho ya Ethiopia ilitangaza kusitisha mapigano hatua iliotoa fursa kwa mashirika ya kiutu kutoa misaada.

**DW**

# Ukraine yazidi kuishambulia Crimea

**KYIV,** UKRAINE

MASHAMBULIZI ya ndege zisizo na rubani yamesikika katika eneo la Crimea na maeneo mengine yanayokaliwa na Russia na kuhofiwa kusababisha madhara makubwa.

Jioni na usiku wa kuamkia jana moshi ulionekana ukitanda angani katika makao makuu ya meli iliyoko Bahari Nyeusi ya Shirikisho la Russia huko Sevastopol.

Shirika la utangazaji la Suspilne la Ukraine, liliripoti asubuhi ya jana tukio hilo pamoja na video kutoka eneo la tukio.

BBC bado haijaweza kuthibitisha mashambulizi hayo.

Vyombo vya habari vya Russia vilisema uvamizi dhidi ya bandari moja magharibi mwa Crimea ulizuiwa siku ya Ijumaa.

Video zilizorekodiwa huko Crimea zilionyesha ulinzi wa anga ya Russia ukikamata shabaha angani juu ya Sevastopol, Yevpatoriya na Zaozerne.

Mamlaka zinazoikalia kwa mabavu Russia zilisema ndege hizo zisizo na rubani ni za Ukraine, lakini hili halijathibitishwa. Kumekuwa na msururu wa mashambulizi dhidi ya maeneo ya jeshi la Russia na vifaa vyake huko Crimea wiki iliyopita, ambayo Ukraine haidai kuhusika.

Maofisa wa nchi za Magharibi walisema mashambulizi hayo dhidi ya Crimea yana madhara makubwa ya kisaikolojia na kiutendaji kwa vikosi vya Russia.

Awali milipuko katika kambi ya anga ya Saki Agosti 9, na mashambulizi mengine yameziweka zaidi ya nusu ya ndege zilizo kwenye meli zilizoko bahari nyeusi kushindwa kufanya kazi.

Wakati huo huo, makombora manne ya Russia yamedunguliwa mashariki mwa Ukraine jana, kulingana na shirika la habari la Ukraine (UNIAN).

Kulingana na ripoti hizo, ambazo zimeonekana inaonyesha vikosi vya ulinzi wa anga vya Ukraine vilinasa makombora manne ya Kalibr kutoka Russia katika eneo la mashariki la Dnipropetrovsk.

"Mwanzo mzuri kutoka kwa jeshi letu," mkuu wa utawala wa kijeshi wa kikanda, Valentyn Reznichenko, alinukuliwa akisema. Aliongeza "Ulinzi wetu wa anga ulidungua eneo la Dnipropetrovsk makombora yote manne ya Kalibr ambayo Warusi walilenga eneo hilo tukufu kwa jeshi letu!"

Kamanda Mkuu wa Kikosi cha Wanajeshi cha Ukraine, Valeriy Zaluzhnyy, aliripotiwa akisema kuwa makombora manne ya S-300 yalitumiwa kuangusha makombora ya Kalibr, karibu na jiji la Dnipro.

Wakati mataifa ya Ulaya yakiendelea kujiondoa katika utegemezi wa gesi kutoka Russia, China imeongeza kasi ya uagizaji wa nishati hiyo kutoka kwa jirani yake na mshirika wake wa karibu. Takwimu kutoka ofisi ya forodha ya Beijing mpaka jana ilionyesha Russia ni msambazaji mkubwa wa mafuta katika kipindi cha miezi mitatu mfululizo.

Mnamo mwezi Julai China iliagiza jumla ya tani milioni 7.15 za mafuta kutoka nchini humo, ni ongezeko la asilimia 7.6 katika kipindi cha mwaka mmoja.

Wakati huo huo, uagizaji wa makaa ya mawe ya China kutoka Ruusia ulipanda kwa kiwango cha juu zaidi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita na kufikia tani milioni 7.42 mwezi Julai ikiwa ni karibu asilimia 14.

China hadi sasa haijashutumu vita vya Russia nchini Ukraine lakini inaendelea kuthibitisha uaminifu wake.

**BBC**




Mwanajeshi wa Russia akilinda kinu cha nyuklia cha Zaporizhzhia ambacho ni kikubwa katika bara la Ulaya. **PICHA: REUTERS**

# Ruto aendelea kukutana na wajumbe

**NAIROBI,** KENYA

RAIS mteule wa Kenya, William Ruto, ameendelea kukutana na wajumbe mbalimbali wanaomtembelea katika ofisi yake rasmi ya naibu rais Karen, jijini Nairobi.

Kando na mikutano ya wajumbe wa viongozi wa kisiasa, wengine kutoka vyama ambavyo havikumuunga mkono katika uchaguzi uliopita, pia amekutana na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa.

Jana alikutana na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Chakula Duniani (WFP), David Beasley.

Kupitia chapisho lake kwenye mitandao ya kijamii, Ruto alisema walijadili hali ya kiangazi kaskazini mwa Kenya na pembe ya Afrika.

Alisema mpango wa serikali ijayo utakuwa kuwapa msaada wakulima kupitia ruzuku ili waweze pia kupata mikopo.

**BBC**

MAKALA

# UMASKINI NA DHANA YA UTEGEMEZI



Na Magabilo Masambu - 0689157789

RAIS wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere amewahi kusema: "Umaskini kupita wote duniani ni kumtegemea mtu mwingine kwa mawazo." Kumtegemea mtu mwingine kwa mawazo maana yake ni kwamba kila jambo unalofikiri kufanya unaona utakosea na mara zote unategemea mtu mwingine akwambie kama uko sahihi au la.

Kuna uhusiano mkubwa sana kati ya umaskini wa mtu na fikra zake. Umaskini unaweza kuwa na tafsiri nyingi lakini kwa leo nizungumzie umaskini wa kushindwa kujimudu katika kutatua changamoto za kawaida za kimaisha, kutoka mtu mmoja, familia na taifa kwa ujumla.

Umaskini wa Afrika ulitokana na kutawaliwa na wakoloni. Kutawaliwa kwetu pia pengine kulisababishwa na umaskini huo huo wa mawazo. Walipotutawala walihakikisha kwanza wametujengea dhana ya utegemezi kwamba sisi wenyewe hakuna jambo tunaloliweza mpaka tuwe tumefanyiwa na wao hata katika mambo ya kawaida kabisa ambayo tungaliweza kufanya wenyewe na walifanikiwa.

Kwa hiyo dhana ya utegemezi ikatuingia zaidi nasi tukaamini kwamba hakuja jambo tunaweza kufanya bila hao jamaa, yaani wakoloni. Jambo hili likawachukiza baadhi ya waasisi wetu wa mataifa ya Afrika. Hii ilimfanya Mwalimu Nyerere hapa kwetu kuja na falsafa ya kujitegemea, akaandika mpaka vitabu kuhusu dhana ya kujitegemea.

Wako wachache walimwelewa wengi hawakuelewa lakini zaidi tunaowategemea wakaona janja yao imeshajulikana na matokeo yake wakapiga vita dhana ya kujitegemea kwa namna mbalimbali. Kutokana na upinzani huo, nchi ikapitia vipindi vigumu vya kiuchumi kiasi cha Mwalimu kuonekana mbaya. Vita ikapigwa ndani na nje fikra za kujitegemea zikafa.

Leo kuna watu wanapata fedha za halali au hata za haramu lakini wanaona hawawezi kuzitunza. Wanaamini kwamba wakikaa nazo watazitumia vibaya, hivyo wanaona njia rahisi ya kuhifadhi ni katika vikundi vya upatu. Hatua hiyo imesababisha siku hizi vikundi hivyo kuwa vingi kila kona. Utasikia wanasema tunatunziana pesa kila baada ya muda fulani tunagawana. Ni kweli kwamba fedha hizo hazizai lakini wanadai wanapata mahali pa kuhifadhia.

Utaratibu huu naweza kuuweka katika dhana ya kutoweza kujitegemea. Maana yake siku vikundi huna na umepata fedha nyingi, huwezi kuzitawala, ndiyo maana pamesikika kelele za baadhi ya wastaafu ama kutapeliwa fedha zao au kuzitumia vibaya na ndani ya muda mfupi unakuta zimeisha na hakuna alichofanya cha maana utegemezi!

Dhana hiyo hiyo imeenda mbali zaidi mpaka katika ngazi ya taifa. Nasema hivi kwa sababu sasa hivi naandika makala hii nikiwa huku Kanda ya Ziwa, nimepita mkoa wa Mwanza nikaenda Mkoa wa Mara. Jambo moja ambalo limenishangaza sana ni kuona tatizo la maji ambalo limekuwapo miaka nenda rudi bado katika karne hii lipo. Kilichonishangaza si kutokuwapo maji safi ya kunywa na matumizi mengine ya nyumbani, bali ni ukaribu wa maji kutoka Ziwa Victoria na vijiji vyenye shida ya maji.

Mfano nimekuwapo maeneo ya Bugando. Ukiwa hapo unayaona maji ziwani mita chache kabisa lakini watu wana mgawo wa maji, kwa juma yanatoka si siku zote. Nimekwenda Mara Wilaya ya Bunda vijiji kama Namuhula, Isanju, Bulenda Bufwe na Igundu hawana maji. Inabidi kinamama waamke usiku wa manane ama watembee umbali mrefu waende ziwani kuyafuata au wakavizie sehemu ambazo zinachimbwa madini kama Namuhula ili wachote maji ambayo si salama kwa afya zao.

Nimepata taabu kuelewa kwamba hivi ni kweli kupata maji kwenye mabomba ambayo yanaweza kuchukuliwa mita chache tu kutoka ziwani tunahitaji wazungu watufanyie hilo? Nilipowauliza wakazi wa Namuhula wakaniambia kuna mradi wa maji katika awamu ya tano ulianzishwa pale Isanju wakachimba mitaro wakaweka mipira mpaka kwenye mabomba ya vijiji, lakini mpaka leo hawajui kinachoendelea!

Najaribu kufikiri kama Kanda ya Ziwa ambako maji yako mita chache sana kuwafikia wananchi, yanashindwa kufika, vipi kuhusu maeneo mengine ambayo vyanzo vyake viko mbali? Lakini tukumbuke Tanzania tumebarikiwa kuwa na vyanzo vingi vya maji, tuna maziwa na mito mingi, tukiachana na matumizi ya nyumbani je, kwenye kilimo tunayatumiaje? Wizara ya Kilimo ina mpango gani kuhusu kuyatumia maji tuliyo nayo katika kuzalisha chakula cha kutosha? Au tuwe sawasawa na wengine duniani wenye taabu ya maji?

Natambua juhudi za serikali katika kuhakikisha majisafi na salama yanapatikana kila kona ya nchi lakini wawakilishi wetu mnafanya juhudi gani? Maana katika baadhi ya maeneo nimezungumza na wananchi wamenieleza kwamba hata wawakilishi wao hawajawahi kuonekana na maoni ya wengi wanasema tunawasubiri katika uchaguzi mkuu mwaka 2025.

Ni muhimu sana kwa yale yaliyoko ndani ya uwezo wetu, tuyafanye kwa kushirikiana na wananchi wenyewe. Tusiwafanye wananchi pia wawe wanasubiri kila kitu kifanywe na serikali bali washirikishwe vyema ili watoe sehemu ya nguvu zao na fedha ya serikali ifanye sehemu. Tuondoe dhana ya utegemezi ili kufuta umaskini badala ya kutumia muda mwingi kwenye maji wakatumie kuzalisha ili wazisaidie familia zao.

0689157789
magabilomjalifu@gmail.com
ARUSHA-TANZANIA

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Chakubanga aliyejiita John Smith kisha akaimbwa na Majirani Rajab



Na Adam Fungamwango

UNAWEZA ukadhani ulikuwa utunzi wa kufikirika lakini huu ni wa kisa cha kweli ambacho kilitokea kwenye maiaka ya 1980. Kila kilichoimbwa kwenye wimbo huu ni cha kwenye kabisa na Marijani Rajab alimtungia mmoja wa ndugu zake wa karibu.

Mashabiki waliupa majina mbalimbali kama 'Awe Mwana', 'Chakubanga', 'Mwana Vibaya', lakini jina lake halisi ni 'Mwana Acha Ujinga'.

Haya mambo ya baadhi ya vijana kwenda nchi za nje, wakirejea wanabadilika hata tabia zao yalianza zamani sana. Iwe waliokwenda kwa ajili ya masomo au kazi ya ubaharia, mara nyingi waliporejea nchini walikuwa na mambo mengi, mbwembwe na vituko vilivyowashangaza wengi.

We angelia tu, leo hii baadhi ya watu hawajaenda hata Ulaya, wako hapa hapa Bongo lakini wakipata vyeo tu 'nanga inapaa'. Ndugu zake, majirani na marafiki anawaona takataka. Ndiyo itakuwa kwa wale waliokwenda Ulaya, tena miaka hiyo ya 1980 kurudi nyuma ambapo ilikuwa ngumu mno tofauti na sasa? Zamani ukiona mtu kaenda Ulaya, ujue amezamia meli au amepelekwa na serikali kusoma kwa ajili ya kulisaidia taifa.

Baadhi yao badala ya kulisaidia taifa baada ya kusomeshwa na pesa za serikali, waligeuka vituko. Serikali ilisomesha wananchi wake ili waje kulisaidia taifa na wanasaidia wananchi ambao wengi ni masikini. Baadhi yao wakaja na vyeti, wakawa wanatamba navyo tu badala ya kukionyesha kile ambacho walichosomea kwa kuwapa elimu wananchi nini cha kufanya kutatua changamoto zao.

Mfano unaposoma mjini, ukirejea kijijini, badala ya kuona watu wote mbumbumbu, unatakiwa uwape elimu kuwa kumbe maji ya kisima wanayokunywa inabidi wachemshe. Watu wengi wanakufa kijijini si kwamba wanarogwa ila ni ugonjwa wa malaria na kwa maana hiyo inabidi waanze kuua mazalia ya mbu.

Huyo ndiye msomi. Anayesomeshwa na pesa za nchi, kijiji au ukoo na anarudi kuwa msaada kwao kwa kuwafundisha vitu vingi ambavyo hawakuvifahamu.

Sasa kuna wasomi ambao badala ya hivyo, wao wanapita kwa mikogo, kudharau watu, kuonyesha kuwa amesoma sana, na wengine wanakwenda mbali zaidi wanawakana mpaka wazazi wao.

Hii ya kukana wazazi naona hii miaka ya kuanzia 1990 imepungua sana. Wamebaki wale wa dharau na mikogo tu lakini nyuma ya hapo, hasa waliokwenda Ulaya au kuwa na maisha ya juu, walifikia pabaya na kuwakana hata wazazi wao na hata hawataki kurudi walipozaliwa.

Wimbo huu wa Marijani ni uthibitisho wa hilo na tutaenda nao kuonyesha kijana huyo alivyofanya vituko baada ya kurejea kutoa Ulaya, watoto wa mjini zamani walikuita 'ng'ambo'.

"Leo kijana ninasema eee, hayo mambo yako unayofanya eee, mwisho wake mwana mambo yanakuwa mabaya, wala usidanganyike na cheo ulichopata, kudharau wazazi kuhadaika na dunia, mwana vibaya, vibaya mwana vibaya aaa.

Fikiri kwanza ulikotoka eee, usijifanye huna baba wala mama, waliokulea kwa tabu nyingi na mashaka, waliokusomesha bwana ukahitimu mafunzo, mbona unawanyanyasa na matusi kuwatukana, mwana vibaya ee, vibaya mwana vibaya aaa."

Huyu jamaa pamoja na kwamba baba na mama yake waliuza ufuta na karanga kwa ajili ya kumsomesha ili aje kuwasaidia baadaye amegeuka. Amekuwa akiwadharau na kuwatukana, kisa hawajasoma na ni masikini.

"Mambo ya ajabu uliyofanya, ulipochaguliwa kwenda ng'ambo, uliporudi bwana na jina umebadilisha, jina lako Chakubanga, ukajiita John Smith na mwendo umebadili bega moja umelishusha, mwana vibaye ee, vibaya mwana vibaya aaa.

Mpaka sasa nyumbani hufiki, umefikia kwa marafiki, ati unasema kuna vumbi jingi sana, wala hukumbuki baba, humo ndimo ulimozaliwa, ugali na kisamvu ndicho kilichokukuza, mwana vibaya ee, vibaya mwana vibaya aaa."

Utembeaji wa kushusha bega moja ulikuwa maarufu sana zamani kwa vijana watoto wa mjini, hasa wale mabaharia, waliozamia meli wakati huo na kufanikiwa kurejea nchini wakiwa wamefanikiwa kupata maisha mazuri, wakati huo wakiita 'wameukata'.

Jamaa kaenda Ulaya, aliporudi kila kitu kimebadilika, amebadilisha jina na mwendo, hataki kurudi kwao kwa sababu ni duni. Msomi kama yeye hawezi kukaa kwenye kibanda 'mbavu za mbwa'. Badala yake amefikia kwa marafiki, wengine walikuwa wanafikia hotelini.

"Mama yako kakutafuta eee, mzee wa watu kahangaika ee, kakusaka mama kwa bahati kakuona, ulipomuona mama, ukajifanya humjui mama, unawauliza marafiki, wamuulize ana shida gani, anajibu Chakubanga, unamwambia hapa hayupo, wewe siyo chakubanga, ila wewe ni John Smith, mama kaondoka, analia mama analia, anaona uchungu, analia mama analia aaa."

Damu nzito kuliko maji, mama baada ya kusikia kijana wake amerejea kutoka Ulaya na amefikia kwa rafiki zake, akamtafuta mpaka akamuona.

Jamaa alipomuona akajifanya hamjui, akawauliza marafiki zake, bi mkubwa amefuata nini hapa? Mama anajibu nimemfuata mwanangu Chakubanga, jamaa anawaambia wenzake, mwambieni hakuna mtu kama huyo hapa. Mama anashangaa na kuuliza wewe siyo Chakubanga? Kijana anamwambia hajawahi kuitwa Chakubanga, yeye ametoka ng'ambo bwana anaitwa John Smith.

Baada ya tukio hilo mama anaondoka huku akilia kwa uchungu. Hebu fikiria, baada ya tukio hilo nini kitafuata?

Kama nilivyosema hicho kilikuwa kisa cha kweli cha mmoja wa ndugu wa Marijani, akakitungia wimbo kudhihirisha kuwa wanamuziki wa zamani walikuwa mahiri kwa kutunga matukio mengi ya kweli, yaliyo ndani ya jamii na yataendelea kutokea kwenye uso wa dunia. Na ndiyo maana nyimbo zao hazichuji.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

PRINCE Petit kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja tu na walipomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile, badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoena na mtu yeyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane tu alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani Anapofika umri wa miaka 25, baba yake mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

# Mwisho wa Mauaji-15

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

KUMBE ulitaka kuniua mama yako." Hidaya aliongeza huku akianza kuangua kilio.

Hasnat alitaka kumbembeleza mama yake. Prince akamzuia. "Mwache kwanza, kuna kitu hapa si cha kawaida."

Hata Hasnat aliamini hivyo. Akajiuliza kwa nini tangu jana hakumtambua, na hadi leo hakuweza kumtambua hadi walipopeana mikono.

Dakika tano zilipita. Hidaya akanyamaza na kuanza kujifuta machozi.

"Mama uko sawa?" Hasnat alimuuliza.

"Niko sawa mwanangu, ila nimeumia sana."

"Mama kwani imekuaje mbona mimi sielewi?" Binti akauliza tena, huku Prince akiwa amekaa kwenye kiti akionekana ana mawazo mengi kwani huenda kuna kitu ambacho hakijui kimemzunguka.

"Hasnat, nikwambie tu huyo hapo ni kijana niliyemlea mwenyewe, tangu anazaliwa."

"Umemjuaje? Mbona tangu jana hujamtambua hadi leo hii, muda wote huu hujamtambua kwa nini?"

Ni swali ambayo hata Prince alikuwa anataka kumuuliza baadaye. Hasnat amemsaidia.

"Nisikilizeni wanangu, sijakujua muda wote huu. Kitu kilichokuja kunijulisha ni makovu mawili ya mkononi, pamoja na hilo kovu dogo mdomoni. Mwanzoni sikutilia maanani, lakini uliponipa mkono nikaona makovu mawili tofauti kwenye mkono wake wa kulia, nikakuangalia hapo pembeni mwa mdomo, nikawa kama namkumbuka mtu fulani, baadaye nikagundua huyu atakuwa ni Prince. Na si hapo tu, hata kifuani hapo, amevaa shati tu, lakini kuna kovu dogo analo kama kweli ni Prince."

"Ndiyo mama ninalo, kwani vipi, inaonekana unanifahamu sana?" Prince akadakia.

"Ndiyo nayafahamu makovu hayo uliyapata ukiwa mdogo, ndiyo unaanza kutembea, ni makovu yaliyotokana na kuungua na uji ambao ni mimi mwenyewe ndiye niliyekuwa nimeuinjika, ndiyo maana nayajua ulivyoungua, jinsi tulivyohangaika hadi ukapona na ukabaki na makovu hayo, ila naona yamekuwa yakipungua ukubwa kadri unavyozidi kukua




**"Prince, kabla sijakwambia chochote, nataka unielezee moja baada ya jingine maisha yako yote uliyokuwa ukiishi tangu pale ulipoanza kupata akili na kuhafamu zuri na baya, na ni nani aliyekutuma uje kuniua? Na kwa nini? Na kama uliua mwingine kabla ya kuja kuniua mimi? Usiogope tena, mimi ni mama yako."**

mwanangu."

Prince aliendelea kuchanganyikiwa, baba yake mzazi mzee Pokwa anamwambia mama yake ameuawa na maadui waliokuwa wamenyang'anya shamba la wazazi wake. Pia anamtuma kulipa kisasi cha wote waliomuua mama yake. Mmoja wa aliomtuma kumuua ni huyu Hidaya. Leo hii huyu alitakiwa kuuawa anamwambia anamfahamu tena kwa kumuonyesha alama za makovu ambazo hata mwenyewe hakujua na wala hakuwahi kumuuliza baba yake yametokana na nini. Kila kitu anachokisema kiko sahihi. Na vingine hakupata kuvijua.

"Sielewi mama, unataka kuniambia kuwa wewe ndiye mama yangu mzazi?" Prince akauliza ili apate uhakika.

"Prince, kabla sijakwambia chochote, nataka unielezee moja baada ya jingine maisha yako yote uliyokuwa ukiishi tangu pale ulipoanza kupata akili na kuhafamu zuri na baya, na ni nani aliyekutuma uje kuniua? Na kwa nini? Na kama uliua mwingine kabla ya kuja kuniua mimi? Usiogope tena, mimi ni mama yako."

Prince alikuwa kama hamwelewi hivi Hidaya. Muda si mrefu alimwambia Hasnat ndiye mtoto wake pekee, vipi hata dakika mbili hazijapita aseme yeye ni mtoto wake pia? Akaurudisha ubongo wake dakika kadhaa nyuma alivyouliza.

"Hivi mama, Hasnat huyu ni wa ngapi?"

"Mhh, we mwanangu acha tu. Ni huyo huyo mmoja tu, kwanza na wa mwisho na haiwezekani tena mimi kupata mtoto."

Akajikumbusha na baadaye akaanza kuwaza. "Iweje sasa ageuke na kusema ni mama yangu?"

Ghafla akakumbuka anatakiwa aeleze historia yake huko nyuma kwa ufupi, kabla ya Hidaya kumwambia anachokifahamu kuhusu yeye.

"Mama, mimi nimeanza kupata akili, mtu niliyeanza kumfahamu ni baba yangu mzazi tu. Sina mama, wala dada, au ndugu yeyote. Nimelelewa kwa kuchungwa sana nisionane na watu. Nyumbani nilikuwa naishi peke yangu. Lakini wakati huo nilikuwa nafundishwa kulenga shabaha. Yaani napata akili, tayari nilishaanza kushika bastola. Sijua ni kwanini, lakini kwa sababu ndiyo nilikuwa napata akili nikajua ndiyo mfumo wa maisha ya watu wote duniani. Nilipokuwa mkubwa, ndipo baba aliponiambia maana ya kunifundisha kulenga shabaha. Akaniambia mama yangu aliuawa na watu ambao waligombana na wazazi wake kuhusu shamba.

Walimuua wakati akienda mahakamni akiwa na hati. Alipigwa risasi gari ikiwa kwenye foleni, wakachukua na nyaraka hizo. Wakaenda kuzibadilisha, wakamiliki shamba kubwa la mama."

Hidaya alionekana kusikiliza kwa makini habari hiyo. Hasnat pamoja na kusikiliza, lakini alionekana kushangaa pia.

"Basi mama, baba akaniambia wale watu walikuwa wananitafuta pia mimi ambaye niliachwa kichanga ili waniue kwa sababu alihofia nikiwa mkubwa naweza kulipiza kisasi. Ikawa naishi kwa kufichwafichwa. Na kweli nilipokuwa mkubwa baba akanipa kazi ya kuwaua wote waliohusika. Nilianza kumuua Sabri, akaja Hussein, baadaye nikawamaliza Nassor na Hassan kwa pamoja kwenye ajali. Wa mwisho ulikuwa wewe mama ili nimalize wote waliohusika." Akamaliza na kushusha pumzi ndefu.

"Ina maana huyo baba yako alikwambia mimi nilihusika kwenye kumuua mama yake mzazi?"

"Ndiyo."

"Pole sana mwanangu. Narudia tena kukupa pole. Kiufupi ni kwamba mimi nawafahamu wote uliowaua.

Nilikuwa nasikia vifo vyao, lakini nilikuwa sijajua sababu haswa, mara wengine kwa kupigwa risasi, wengine ajali ya gari, sikujua kama kuna hili unaloniambia. Ukweli mwanangu umeua watu muhimu sana kwenye maisha yako."

Hilo lilimshtua Prince. Kila hatua anayopiga inakuwa ngumu zaidi. Anataka kufahamu kama Hidaya ni mama yake mzazi. Lakini anaongezewa kwa kuambiwa aliowaua walikuwa watu muhimu sana kwake na kwenye maisha yake. "Kwa nini. Kwani kuna nini?" Akajiuliza mwenyewe.

Sura na macho yake yalionyesha kabisa kama ni mtu aliyechanganyikiwa na haelewi mambo yanakwendaje.

"Ina maana baba alikuwa ananidanganya?"

"Ndiyo, huyo baba yako kakuingiza mkenge. Uliowaondoa kwenye uso wa dunia ndiyo walikuwa msaada mkubwa kwako. Ulikuwa unajitumbukiza kisu mwenyewe tumboni. Hata mimi ni msaada kwako na ndiyo maana ilikuwa pia niuawe. Ashukuriwe Mungu umeniacha hai, tena kwa sababu ya Hasnat. Vinginevyo nisingekuwa hai. Na usingefahamu chochote kuhusu hili hadi unakuwa mzee na unakwenda kaburini."

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# Zuchu kwa kuzuga balaa

ILIKUWA kauli ya utani, lakini mashabiki wanachukulia tofauti, kufuatia msanii wa muziki wa kizazi kipya, Zuchu kumjibu bosi wake kuhusu fidia ya kujitoa WCB endapo atataka kufanya hivyo.

Zuchu, kupitia mahojiano na Wasafi TV, amesema hana shida kulipa bilioni ya kulipa kuvunja mkataba, lakini bado yupo sana ndani ya lebo hiyo.

Diamond wakati akimjibu shabiki aliyemuuliza Zuchu atalipa kiasi gani cha pesa akitaka kujiondoa katika lebo hiyo, alisema atatakiwa kulipa Sh. bilioni 10.

# Mwijaku hatimaye alainika kwa Diamond

MWIGIZAJI wa filamu na mchekeshaji, Mwijaku ameonekana akiwa ndani ya gari la mwanamuziki nyota na Mkurugenzi wa Wasafi, Diamond Platnumz, huku akiliponda kiaina kwamba linapiga kelele.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Mwijaku aliweka video fupi akionekana akiwa ndani ya garo la Diamond aina ya Rolly Royce, pamoja na Baba Levo na Zuchu.

"Nimekuja kuona ndani kama limepakwa rangi, angalia usipige breki kwa sababu linapiga kelele," amesikika Mwijaku akimwambia Diamond.



Msanii huyo asiyeshiwa vituko alipanda gari hilo baada ya hafla ya kutiliana saini mkataba wa Wasafi Bet kudhamini mashindani ya Ndondo Cup.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### YAMKATAA RONALDO

MWENYEKITI wa Borussia Dortmund, Hans-Joachim Watzke amekanusha uvumi unaohusisha klabu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga na mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo, 37, akisema hakuna mawasiliano yoyote na nyota huyo wa Manchester United. ***(Mirror)***

### FOFANA KUTOHUSISHWA

MLINZI wa Leicester City, Mfaransa Wesley Fofana, 21, ameomba kutohusika katika mchezo dhidi ya Southampton wikiendi hii baada ya kuhusishwa na Chelsea. ***(Guardian)***

### CASEMIRO SAFI MAN

KLABU ya Manchester United imefikia makubaliano na Real Madrid kumsajili kiungo wa kati wa Brazil, Casemiro, 30 kwa dau la hadi pauni milioni 70. ***(BBC Sport)***

### PEPE ATAKIWA NICE

KLABU ya Nice ya Ufaransa iko kwenye mazungumzo na Arsenal kuhusu kumnunua kwa mkopo mshambuliaji wa Ivory Coast, Nicolas Pepe, 27. ***(Athletic)***

### HOJBJERG KUMRITHI CASEMIRO

REAL Madrid wanafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Tottenham Hotspur na Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg, 27, kuchukua nafasi ya Mbrazili anayeondoka Casemiro, 30, ambaye amekubali mkataba na Manchester United. ***(Telegraph)***

### SAKA ATASAINI

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta ana imani winga wa England, Bukayo Saka, 20, atasaini mkataba mpya licha ya kuwaniwa na Manchester City. ***(MailOnline)***

### KUDUS NA EVERTON

KLABU ya Everton iko tayari kumsajili Mohammed Kudus, 22, kwa mkopo kutoka Ajax kwa nia ya kufanya uhamisho wa kiungo huyo wa kati wa Ghana, kuwa wa kudumu. ***(Sky Sports)***

### GNONTO AWANIWA

LEEDS United wanalenga kukamilisha dili la kumnunua Willy Gnonto, 18, kutoka FC Zurich, kwa pauni milioni 4 huku mshambuliaji huyo wa Italia akiingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake. ***(MailOnline)***

### ZIYECH KUREJESHWA

AJAX pia wanataka kumrejesha kiungo wa Morocco, Hakim Ziyech, 29, kutoka Chelsea ikiwa Mbrazil Antony, 22, atajiunga na Manchester United. ***(90min)***


### ANTONY NA MAZOEZI

ANTONY alifanya mazoezi peke yake Ijumaa baada ya klabu hiyo ya Uholanzi kukataa ofa ya pauni milioni 67 kutoka Manchester United. ***(Mail)***

### MAGUIRE ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA wameuliza kuhusu kupatikana kwa mlinzi wa Manchester United na England, Harry Maguire, 29, kwa ajili ya makubaliano ya kubadilishana ambayo yatamfanya mshambuliaji wa Marekani Christian Pulisic, 23, kwenda upande wa pili. ***(Mail)***

## DONDOO SOKA MAGAZETI ULAYA



# AUBAMEYANG TAYARI KUTUA CHELSEA

**●●● Uhamisho wake kumhusisha Marcos Alonzo ambaye amekuwa akiwaniwa na Barca...**

**LONDON,** England

PIEER-Emerick Aubameyang yuko tayari kujiunga na Chelsea kwa ofa ya fedha pamoja na kubadilishana wachezaji inayomhusisha Marcos Alonso ikiwa tayari imewasilishwa Barcelona, kwa mujibu wa 90min.

**Nyota huyo mwenye umri wa miaka 33 amekuwa mchezaji wa Barcelona kwa miezi saba pekee baada ya kujiunga na klabu hiyo kwa uhamisho wa bure kutoka Arsenal.**

Lakini muda wake wa kukaa pale Camp Nou unaweza kufikia kikomo huku Kocha Thomas Tuchel akipania kuongeza nguvu kwenye safu yake ya ushambuliaji hapo Stamford Bridge.

Kikao kilichofanyika Alhamisi asubuhi kati ya Chelsea na wawakilishi wa Aubameyang, imefahamika kwamba iliwekwa wazi mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon atakuwa tayari kurejea London kuungana na Tuchel - kocha wake wa zamani katika klabu ya Borussia Dortmund.

Inafahamika kuwa Chelsea sasa wametuma ofa ya kumnunua Aubameyang, ambayo pauni milioni 15 pamoja na Marcos Alonso - mchezaji ambaye miamba hiyo ya Katalunya imekuwa ikimwania.

Makubaliano ya maslahi kibinafsi bado yanahitaji kuafikiwa kikamilifu na Aubameyang, na wakati ofa ya Chelsea iko chini ya bei inayodaiwa kuwa ya pauni milioni 20 ambayo Barcelona wanataka.

Alonso tayari amefikia makubaliano ya maslahi binafsi na Barcelona na anajiandaa kufanyiwa vipimo vya afya, akijua kwamba muda wake Chelsea unakaribia mwisho.

Kocha Mkuu wa Barcelona Xavi, alikuwa ameeleza nia ya kutaka kumbakisha Aubameyang katika klabu hiyo, licha ya kumsajili Robert Lewandowski kutoka Bayern Munich, lakini hali mbaya ya kifedha ya klabu hiyo inaweza kuwa sababu nyingine ya kuamua iwapo ofa ya Chelsea itakubaliwa au la.

Kwa sasa, chaguo bora za Chelsea ni pamoja na Kai Havertz na Armando Broja, baada ya Romelu Lukaku kuondoka na kujiunga tena na Inter Milan kwa mkopo na Timo Werner kwenda klabu yake ya zamani, RB Leipzig.

Mmiliki mwenza Todd Boehly pia anafanya kazi ya kutaka kumnunua mlinzi wa Leicester, Wesley Fofana kwa fedha nyingi, huku harakati za The Blues kumnunua fowadi wa Everton, Anthony Gordon bado zinaendelea.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
LILLE
VERSUS
PARIS ST GERMAIN
1 | 5.49
X | 4.26
2 | 1.52

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RONALDINHO: JESUS ATAWIKA SANA ARSENAL



**LONDON,** England

GWIJI wa soka wa Brazil, Ronaldinho amedai Gabriel Jesus atalipa 'upendo' alioupata Arsenal kwa kuwa mmoja wa wachezaji bora barani Ulaya.

Jesus alifunga mabao 95 katika mechi 236 alizoichezea Manchester City, na kushinda mataji nane makubwa, lakini alijikuta hana nafasi ya kuanza mara kwa mara.

Tangu ahamie Arsenal, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 ameonesha kiwango cha kuvutia kama mchezaji anayeanza mara kwa mara na alihusika moja kwa moja katika mabao yote manne ambayo Washikabunduki hao walifunga dhidi ya Leicester City wikendi iliyopita.

Ronaldinho amekuwa shabiki wa Jesus tangu mchezaji huyo alipohamia England kutoka klabu ya Palmeiras ya Brazil akiwa kijana mdogo.

Lakini amependekeza mchezaji huyo hakupata fursa ya kuonesha ubora wake kule Manchester na sasa atafanya hivyo pale Arsenal.

"Gabriel alipojiunga na Manchester City, nilisema angeendelea kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani," alisema Ronaldinho akinukuliwa na gazeti la Mirror.

"Alipopewa nafasi, alionesha kile alichoweza, lakini akiwa Manchester City hakuwahi kuoneshwa upendo ambao mchezaji wa ubora wake anastahili.



## *Tuchel aanza mazungumzo mkataba mpya*

**LONDON,** England

CHELSEA imeanza mazungumzo na kocha Thomas Tuchel juu ya kuongeza mkataba wake pale Stamford Bridge.

Awali Mjerumani huyo alitia saini mkataba wa miezi 18 aliporithi mikoba ya Frank Lampard Januari 2021, lakini akaongeza muda wa kukaa kwake haraka baada ya kuiongoza klabu hiyo kupata mafanikio ambayo hayakutarajiwa kwa kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Tuchel tena alioongoza Chelsea kumaliza katika nafasi nne za juu msimu uliopita, na amepewa jukumu la kusimamia mabadiliko makubwa ya wachezaji chini ya mmiliki mpya Todd Boehly.

Romelu Lukaku na Timo Werner ni miongoni mwa wachezaji maarufu walioondoka hivi karibuni kule magharibi mwa London, lakini Tuchel anaonekana kuungwa mkono kikamilifu na bodi ya klabu - jambo ambalo limedhihirishwa na uthibitisho wake kwamba mazungumzo kuhusu mkataba mpya yanaendelea.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# JULIO AMTABIRIA LUSAJO UFUNGAJI BORA

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Namungo FC, Jamhuri Kihwelo 'Julio' amesema kwa moto wa mshambuliaji wao, Relliants Lusajo amekuwa wa moto zaidi msimu huu na anaweza kuibuka kuwa mfungaji bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Lusajo ni kinara wa mabao ndani ya Namungo FC na anaongoza kwenye orodha ya washambuliaji baada ya kutikisa nyavu mara tatu katika michezo miwili ya ligi.**

Kwa mujibu wa Julio kasi na moto aliokuwa nao mshambuliaji wao huyo ana matarajio makubwa ya msimu huu nyota huyo kutwaa tuzo ya mfungaji bora mwishoni mwa msimu.

Alisema msimu uliopita alikuwa katika washambuliaji hatari na kuwania kiatu hicho, alishindwa kwa sababu ya kupata majeruhi na kushindwa kufanya vizuri na kutoingia katika vita vya mfungaji bora.

"Msimu huu tunaomba Mungu, Lusajo aweze kuwa imara na kutokuwa majeruhi nina imani kwa moto aliouwasha anaenda kuchukua kiatu chake cha mfungaji bora," alisema Julio.

Alisema msimu huu ligi imekuwa na ushindani mkubwa na katika kuhakikisha wanatumia mapumziko ya kupisha timu ya Taifa kucheza michuano ya CHAN, kuandaa timu yao kuwa imara zaidi.

"Tunategemea kuwa na Namungo tofauti kabisa, baada ya kutumia mapumziko haya ya kupisha timu ya Taifa kucheza CHAN, tutaendelea mazoezi ya kuendelea tulipoishia katika pre-Season yetu kwa ajili ya kuitengeneza Namungo kuwa tishio zaidi," alisema Julio.





Rais wa Golf Wanawake Tanzania, Sophia Viggo, akipiga mpira wakati wa uzinduzi wa mashindano ya Golf Afrika, yanayotarajia kufanyika hapa nchini mwezi ujao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Zanzibar Heroes kuingia kambini leo*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes), Hemed Suleiman Ali 'Morocco,' ametangaza kikosi cha wachezaji 26 kitakachoingia kambini leo kujiandaa na mchezo wa kirafiki dhidi ya Uganda.

Mchezo huo unatarajiwa kuchezwa Jumatano, Agosti 24, 2022, katika Uwanja wa Amaan, saa moja kamili jioni.

Wachezaji walioitwa kwenye kikosi hicho ni pamoja na Magolikipa, Ahmed Ali Suleiman (Azam) na Sheha Abdullah Ali (Malindi).

Walinzi ni Ibrahim Mohammed Said (KVZ), Salum Khamis Salum (KVZ), Mohammed Othman Mmanga (Polisi Tanzania), Adeyum Saleh Ahmed (Geita Gold), Abdulmalik Adam Zakaria (Namungo), Abdallah Kheir Salum (Azam), Ibrahim Ame (KMC), Ibrahim Abdallah Hamad (Yanga), Ali Hamoud Badru (KMKM), Suwen Abdallah Omar (Selem View) na Omar Haji Omar (Namungo).

Viungo ni Feisal Salum Abdallah (Yanga), Is-haka Said Mwinyi (KMKM), Ahmed Maulid Amour (Tanzania Prison), Abdullaziz Makame (Kagera Sugar), Khalid Habibi Idd (KMKM), Rashid Mohammed Is-haka (KVZ), Hassan Haji (Zimamoto) na Ilyasa Suleiman Mohammed (KMKM).

Washambuliaji ni Matheo Anthony Simon (KMC), Maabad Maulid Maabad (Coastal Union), Ibrahim Abdallah Mkoko (Namungo), Abdulnassir Assa Gamal (Mlandege) na Mundhir Abdallah Vuai (Kipanga).

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 21/08/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1158 | BATE Borisov vs Dnepr Mogilev | 1.10 | 7.46 | 17.67 |
| 14:00 | 2393 | Strasbourg vs Reims | 1.78 | 3.47 | 4.43 |
| 14:00 | 5810 | Bristol City vs Cardiff | 2.20 | 3.25 | 3.15 |
| 14:30 | 4676 | Guangzhou Evergrande vs Shenzhen | 3.87 | 3.33 | 1.85 |
| 15:00 | 1480 | Khon Kaen United FC vs Ratchaburi | 3.09 | 3.29 | 2.12 |
| 15:00 | 4050 | CSKA Moscow vs Akhmat Grozny | 1.83 | 3.55 | 3.95 |
| 15:00 | 5996 | FK Auda vs FC Riga | 5.89 | 3.73 | 1.51 |
| 15:30 | 5792 | Sparta Rotterdam vs Ajax | 9.40 | 6.00 | 1.24 |
| 16:00 | 1851 | Leeds vs Chelsea | 5.38 | 4.19 | 1.53 |
| 16:00 | 2611 | Clermont Foot vs Nice | 3.51 | 3.36 | 2.03 |
| 16:00 | 3841 | Montpellier vs AJ Auxerre | 2.12 | 3.37 | 3.27 |
| 16:00 | 5055 | West Ham vs Brighton | 2.26 | 3.29 | 2.99 |
| 16:00 | 5538 | Angers vs Brest | 2.26 | 3.32 | 3.02 |
| 16:00 | 5963 | Toulouse vs Lorient | 2.01 | 3.42 | 3.52 |
| 16:30 | 1299 | Eintracht Frankfurt vs FC Koln | 2.00 | 3.55 | 3.35 |
| 17:00 | 1363 | Kapaz vs Gabala | 5.60 | 4.10 | 1.52 |
| 17:00 | 2123 | Randers vs Viborg FF | 2.10 | 3.42 | 3.27 |
| 17:00 | 4630 | Celtic vs Hearts | 1.21 | 6.43 | 11.06 |
| 17:30 | 2634 | Casa Pia Atletico vs Boavista | 2.45 | 3.02 | 2.97 |
| 17:30 | 5834 | Zenit St Petersburg vs Torpedo Moscow | 1.14 | 7.39 | 14.99 |
| 17:45 | 3670 | Waalwick vs Feyenoord | 7.61 | 5.21 | 1.32 |
| 18:00 | 1223 | Wolfsberger AC vs Austria Vienna | 2.45 | 3.15 | 2.66 |
| 18:05 | 3239 | Rennes vs AC Ajaccio | 1.42 | 4.32 | 7.24 |
| 18:30 | 1592 | Newcastle vs Manchester City | 6.53 | 4.48 | 1.42 |
| 18:30 | 2171 | VfL Bochum vs Bayern Munchen | 12.01 | 7.40 | 1.16 |
| 18:30 | 3161 | SuperSport Utd vs Orlando Pirates | 3.71 | 3.01 | 2.09 |
| 18:30 | 3630 | Athletic Bilbao vs Valencia | 1.68 | 3.69 | 4.95 |
| 19:00 | 2261 | Lillestrom vs Sandefjord | 1.31 | 5.24 | 8.26 |
| 19:00 | 2583 | Haugesund vs Molde | 3.76 | 3.82 | 1.83 |
| 19:00 | 3487 | Aalborg vs Brondby | 2.36 | 3.37 | 2.82 |
| 19:00 | 4658 | Valerenga vs Tromso | 1.67 | 3.81 | 4.71 |
| 19:00 | 4746 | Stromsgodset vs Jerv | 1.33 | 5.23 | 7.65 |
| 19:00 | 5380 | Radnik Surduluca vs Radnicki Nis | 2.60 | 3.18 | 2.50 |
| 19:15 | 5288 | Basaksehir vs Kayserispor | 1.55 | 3.96 | 5.61 |
| 19:30 | 4101 | Napoli vs Monza | 1.34 | 5.01 | 7.41 |
| 19:30 | 4195 | Empoli vs Fiorentina | 3.50 | 3.65 | 1.92 |
| 19:30 | 4560 | Zira vs FK Sumgayit | 1.84 | 3.34 | 3.89 |
| 19:55 | 4409 | Istra vs HNK Rijeka | 3.57 | 3.32 | 1.93 |
| 20:00 | 1927 | FC Krasnodar vs Gazovik Orenburg | 1.76 | 3.75 | 4.10 |
| 20:00 | 5943 | Sporting Braga vs Maritimo | 1.37 | 4.71 | 7.42 |
| 20:30 | 1572 | Atletico Madrid vs Villarreal | 1.88 | 3.44 | 4.04 |
| 20:30 | 3913 | Aris Salonica vs Levadiakos | 1.42 | 4.22 | 7.63 |
| 21:00 | 2021 | Rosenborg vs Aalesunds | 1.39 | 4.72 | 7.03 |
| 21:00 | 5376 | Vasas SC vs Budapest Honved | 2.42 | 3.30 | 2.61 |
| 21:45 | 3099 | Besiktas vs Fatih Karagumruk | 1.58 | 4.02 | 5.22 |
| 21:45 | 3845 | Bologna vs Verona | 2.12 | 3.44 | 3.14 |
| 21:45 | 4035 | Atalanta vs AC Milan | 2.69 | 3.34 | 2.44 |
| 21:45 | 5931 | Lille vs Paris St Germain | 5.49 | 4.26 | 1.52 |
| 23:00 | 1924 | Tenerife vs Lugo | 1.61 | 3.44 | 5.99 |
| 23:00 | 4898 | Real Sociedad vs Barcelona | 3.15 | 3.39 | 2.19 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Agosti 21, 2022

Nipashe



Aubameyang tayari kutua Chelsea UKURASA 21

# Yanga SC yatakata kwa Coastal

## Bao la Morrison latolewa maalumu kwa shabiki aliyefariki kwa ajali, huku Mayele...

**Na Adam Fungamwango**

BERNARD Morrison raia wa Ghana, alifunga bao lake la kwanza kwa Yanga tangu arejee kwenye timu hiyo akitokea Simba, dakika ya nne tu ya mchezo kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union, huku Fiston Mayele akifunga bao lake la pili kwenye mechi hiyo, Yanga ikishinda mabao 2-0.

**Mechi hiyo iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid Arusha, ikiwa ni ya pili kwa timu hizo tangu zilipokutana Julai 2, mwaka huu, kwenye fainali ya Kombe la FA.**

Timu hizo zilitoka mabao 3-3, Yanga ikibeba ubingwa kwa mikwaji 4-1 ya penalti.

Bao la kwanza lilikuwa ni maalum kwa shabiki wa timu hiyo Dada Hadija aliyefariki kwa ajali ya gari Bagamoyo mkoani Pwani, majeruhi na mashabiki wote waliokuwamo kwenye ajali hiyo walikuwa wakitokea Dar es Salaam kwenda Arusha kuangalia mechi hiyo.

"Goli letu la kuongoza lililofungwa na Bernard Morrison ni maalum kwa msiba wa mashabiki wetu Dada Hadija na wote waliopata ajali jana (juzi). Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa nguvu," ilisomeka taarifa ya Yanga kupitia ukurasa wake wa facebook.

Ilikuwa ni kazi mzuri iliyofanywa na Jesus Moloko ambaye aliwazidi mbio mabeki wa Coastal Union, akamchungulia mfungaji aliyekuwa amejiweka kwenye nafasi nzuri na kuuweka nyavuni kirahisi, huku kipa Mahamoud Mroivili akiwa amevutika.

Yanga ndiyo iliyotawala kwa kiasi kikubwa kipindi cha kwanza, huku Coastal Union ikizuia na kufanya mashambulizi ya kushtukiza, lakini yaliyokuwa ya hatari na kama wangekuwa makini, si tu kwamba ingesawazisha kabla ya mapumziko, lakini hata ingeweza kupata mabao mawili.

Kocha Mkuu wa Yanga Nasreddine Nabi alilazimika kufanya mabadiliko ya lazima dakika 25 tu ya mchezo kwa kumtoa Moloko aliyeumia na kumwingiza Dickson Ambundo.

Bakari Mwamnyeto nusura aizawadie Coastal Union bao alipojichanganya na kipa wake Abutwalib Mshery akitaka kuokoa krosi na Nimuboma beki wa zamani wa Simba ambaye alionekana kucheza vema kwenye mechi ya jana, mpira ukatoka sentimeta chache langoni.

Nimuboma tena, akiwa mita 30 aliupata mpira uliokuwa umeokolewa vibaya na mabeki wa Yanga akatandika 'mashine' kali iliyopanguliwa kwa ustadi na Mshery na kuwa kona ambayo haikuzaa matunda.

Stephane Aziz Ki aliupata mpira akiwa nje ya eneo la hatari la Coastal akaachia shuti kali, lakini kipa Mroivili, raia wa Comoro akakaa imara kwa kudaka kwa ustadi dakika tatu kabla ya mapumziko.

Baada ya kuona hakukuwa na mashambulizi ya maana, Kocha Nabi alifanya mabadiliko mengine dakika ya 55, alipomtoa Heritier Makambo na kumwingiza Mkongomani mwenzake Fiston Mayele ambaye kwa mara ya kwanza jana alianzia benchi.

Dakika zake 12 tu uwanjani tangu kuingiza zilitosha kuipatia bao la pili Yanga, ikiwa ni dakika ya 67 ya mchezo huo.

Krosi iliyopigwa kutoka Magharibi mwa uwanja, ilikwenda upande wa Mashariki na kurudishwa kwa kichwa na Djuma Shaaban ukawa unazagaa juu ya lango la Coastal Union. Wakati mabeki wa Coastal Union wakizubaa kuruka, Mayele alionekana kuuhitaji zaidi kuliko wao, akaenda juu na kuukwamisha wavuni.

Yanga sasa ina pointi sita na mabao manne, ikiwa imeruhusu bao moja, Coastal ikibaki na pointi zake tatu, baada ya ushindi wa kwanza dhidi ya KMC.

Kwenye Uwanja wa Liti, Singida, Dodoma Jiji ilifungwa mabao 2-1 dhidi ya Prisons yaliyowekwa wavuni na Ismail Mgunda na Jeremiah Juma, Hassan Mwaterema akifunga bao la kufutia machozi.



Wachezaji wa Yanga, wakiongozwa na mshambuliaji, Bernard Morrison wakishangilia kwa ishara ya kutoa mpole kwa mashabiki wao waliopata ajali na wengine kufariki dunia wakati wa mchezo wao dhidi ya Coastal Union uliopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha jana. Yanga ilishinda mabao 2-0. **PICHA: YANGA**

## Simba, TFF zatuma salamu Yanga

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imetupa salamu za pole na rambirambi kufuatia ajali ya mashabiki wa Yanga waliokuwa wakielekea jijini Arusha kushuhudia mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union, iliyotokea juzi saa 2:00 asubuhi maeneo ya Kiwangwa, Bagamoyo mkoani Pwani na kusababisha kifo cha shabiki mmoja aliyefahamika kwa jina la Dada Hadija.

Katika taarifa yake, uongozi wa klabu hiyo umeonyesha kusikitishwa na kifo hicho, huku wakiwapa pole majeruhi wote ili wapone haraka.

"Uongozi wa klabu ya Simba unatoa pole kwa uongozi wa klabu ya Yanga kufuatia msiba wa shabiki wa timu hiyo aliyefariki kwenye ajali ya gari lililobeba mashabiki wa timu hiyo wakiwa wanaelekea jijini Arusha kushuhudia mchezo wa timu yao.

Pia tunatoa pole kwa mashabiki wote waliopata majeraha kwenye ajali hiyo na kuwaombea wapone haraka waweze kurejea kwenye majukumu yao."

Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania, Wallace Karia naye kwa niaba ya (TFF) alitoa salamu za rambirambi na pole kutokana na msiba, pamoja na ajali hiyo.

"Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) ametuma salamu za pole kwa klabu ya Yanga na familia za mashabiki waliopata ajali kwenye eneo la Mwetemo Bagamoyo, Pwani ikisababisha kifo cha shabiki mmoja.

Karia amesema ni sehemu ya mpira wa miguu na ana mchango mkubwa, hivyo kupoteza shabiki kwenye ajali ni jambo la kuhuzunisha sana.

Kwa niaba ya TFF, Rais Karia ametoa pole kwa klabu ya Yanga, familia ya marehemu na kuwatakia kila la heri majeruhi wote wapone haraka.

"Mashabiki hao walipata ajali wakati wakisafiri kwenda Arusha kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha." Ni taarifa iliyotolewa na TFF, ikisainiwa na Ofisa Habari na Mawasiliano, Clifford Ndimbo.

Klabu ya Yanga nayo imetoa taarifa ya kupokea kwa masikitiko taarifa ya ajali hiyo na kusababisha kifo cha shabiki huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >